# MADA

# UHAKIKI WA FANI KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*: NADHARIA YA UMUUNDO

NA

PAMELLA TAMBASI
C50 / 61285 / 2010

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA KISWAHILI

IDARA YA ISIMU NA LUGHA,

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

AGOSTI, 2011

University of NAIROBI Library
0532240 9

# IKIRARI

**Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.**

7/11/2011

PAMELLA TAMBASI
(MTAHINIWA)

TAREHE

**Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu cha Nairobi.**

11/11/11

DKT. KINEENE WA MUTISO
(MSIMAMIZI)

TAREHE

17th November, 2011

BI. HANNAH MWALIWA
(MSIMAMIZI)

TAREHE

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia mume wangu mpendwa bwana Raphael Amuko, aliyetambua umuhimu wa kuelimisha mwanamke katika jamii. Amejitolea mhanga kuhakikisha kuwa nimekamilisha elimu yangu. Vilevile, ninawatabarukia wazazi wangu wapendwa bwana Donald Tambasi na Bi. Esther Tambasi kwa kunipa msingi bora wa kielimu na motisha katika masomo yangu.

Aidha, sitawasahau watoto wangu watatu, Lameck, Evan na Florence, ambao wamenivumilia kwa muda ambao sikuweza kushirikiana nao kwa mambo mengi waliponihitaji.

Ninatumai kuwa wataweza kutambua umuhimu wa masomo katika maisha ya binadamu.

# SHUKURANI

Ninaiunga mkono kauli ya wahenga kuwa, safari ya mbali huanza kwa hatua moja. Hakika safari hii imekuwa ndefu tangu nilipoanza kozi hii. Imekuwa safari yenye panda shuka nyingi ambazo singeweza kukwepa peke yangu. Siwezi kujigamba na kudai kuwa jitihada zangu pekee zingenipa ufanisi pasipo na mchango wa wengine wengi.

Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na nguvu za kukamilisha kozi hii. Bila yeye, singefika nilipofika. Neema zake zanitosha.

Pili, ninatoa shukurani zangu kwa mume wangu mpendwa bwana Raphael Amuko aliyenilipia karo kwa muda huu wote. Amekuwa rafiki wa karibu wa kunishauri maji yalipozidi unga. Isitoshe, alikuwa mwepesi wa kutumwa nilipohitaji msaada wa mbali. Asante sana mume wangu. Mola akukarimie karima.

Aidha, ninatoa shukrani zangu kwa wazazi wangu wapendwa Bw. na Bi. Donald Tambasi. Siku zote walitaka nitie bidii masomoni. Maombi ambayo mama amekuwa akiomba yametimia kwani kufika kwangu nilipo siyo kwa uwezo wangu.

Wahadhiri katika idara ya isimu na lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi wanastahiki shukurani chungu nzima. Mchango wao wa moja kwa moja umenisaidia pakubwa sana katika maisha na masomo yangu. Kuna mambo mengi sana ambayo singeyajua nisingekutana nao. Miongoni mwao ni Prof. John Habwe, Prof. Wamitila Kyalo Wadi, Dkt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Jefwa Mweri na Bwana Mungania.

Shukurani zangu za kipekee ni kwa wasimamizi wangu wawili, Dkt. Kineene wa Mutiso na Bi. Hannah Mwaliwa. Wamekuwa zaidi ya walimu kwangu. Wasomi hawa wameshirikiana nami kama ndugu na sahibu wa karibu. Sitasahau ushauri wao daima dawamu.

Ningependa vilevile kumshukuru Bi. Linah Wambua aliyenishika mkono nilipoanza kozi hii. Amenifaa kwa mawaidha na matini ya kusoma. Hakuchoka kunikaribisha kwake kila nilipohitaji msaada wake kwani hata usiku alinishughulikia. Hakika ninamuombea baraka zake Mwenyezi Mungu.

Ninawashukuru dada zangu Jacqueline,Lilian,Joan,Rachel,Cynthia,Mercy,Carol,Faith na ndugu Nixon na Fred kwa mawaidha yao yaliyonisongesha hatua kadha. Ndugu Yusufu Msandu na familia, yake nawashukuru kwa maombi yenu. Sitasahau ushauri na maombi ya Shemeji yangu Daniel Andere Amuko. Alikuwa na hamu ya kujua kila hatua niliyopitia. Hakika motisha yake imenifanya kujikakamua. Namuombea baraka zake Mola katika kila hatua aichukuayo aushini.

Mwisho, ninawashukuru wenzangu tuliosoma nao. Tulijadiliana na kubadilishana mawazo kuhusu masuala ya kiusomi. Ninashukuru kwa kuwajua na hata kufanya urafiki nao. Wengi walikuwa wachangamfu na wacheshi hata mambo yalipokuwa magumu.

# MUHTASARI

Utafiti huu unahusu uhakiki wa fani katika *Utenzi wa Tambuka*. *Utenzi wa Tambuka* ni utenzi mrefu na wa zamani sana. Utenzi huu ulitungwa na Bwana Athumani bin Mwengo mwaka wa 1728. Utafiti unatekelezwa katika misingi ya nadharia ya Umuundo na unalenga kuhakiki namna mtunzi wa utenzi huu anavyotekeleza muundo wa utenzi wenyewe na namna ubunifu wake unavyomsaidia kuwasilisha ujumbe wake.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita. Katika sura ya kwanza, tunaelezea mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, mipaka na upeo, nadharia tete, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, misingi ya kinadharia na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili, tunajadili misingi ya uhakiki wa fani. Tunafafanua dhana ya fani na vipengele vyake mbalimbali. Sehemu hii inanuiwa kutoa mwongozo kwa utafiti huu kwani inaonyesha vipengele vya kifani vinavyohakikiwa katika sura zifuatazo.

Sura ya tatu inahusu uhakiki wa msuko na muundo katika *Utenzi wa Tambuka*. Katika sura hii, tunachukulia kuwa muundo na msuko ni vipengele vya kifani vinavyohusiana pakubwa na hivyo vinafaa kuhakikiwa kwa pamoja.

Sura ya nne inahusu uhakiki wa Mandhari na Wahusika katika *Utenzi wa Tambuka*. Utafiti unaonyesha namna kipengele cha mandhari kinavyohusiana na ujenzi wa wahusika katika kuwasilisha ujumbe wa utenzi huu. Tumewagawa wahusika wa utenzi huu katika makundi mawili makuu. Kunao wahusika wa Kikristo na wahusika wa Kiislamu. Vilevile, kuna wahusika wa Kikristo wanaobadilika na kuwa Waislamu.

Sura ya tano inahusu uhakiki wa matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Tambuka*. Utafiti unaonyesha namna mtunzi anavyotumia uhuru wa kishairi. Uhuru huo unahusu ukiushi katika matumizi ya lugha. Ukiushi wenyewe ni wa kimofolojia, kisintaksia, kimsamiati na kisemantiki.

Sura ya sita ya tasnifu hii inahusu tathmini na mapendekezo ya utafiti zaidi. Tunarejelea madhumuni ya utafiti pamoja na nadharia tete.

# YALIYOMO

Mada ..................................................................................................... i

Ikirari..................................................................................................... ii

Tabaruku..................................................................................................... iii

Shukrani..................................................................................................... iv

Muhtasari..................................................................................................... vi

Yaliyomo..................................................................................................... viii

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

1.0 Utangulizi..................................................................................................... 1

1.1 Tatizo la utafiti..................................................................................................... 2

1.2 Malengo ya utafiti..................................................................................................... 3

1.3 Sababu za kuchagua mada hii..................................................................................................... 4

1.4 Upeo na mipaka..................................................................................................... 5

1.5 Nadharia tete..................................................................................................... 5

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii..................................................................................................... 6

1.7 Msingi wa nadharia ya utafiti..................................................................................................... 7

1.8 Mbinu za tafiti..................................................................................................... 10

1.9 Hitimisho.....10

## SURA YA PILI

## MISINGI YA UHAKIKI WA FANI

2.0 Utangulizi.....11

2.1 Dhana ya Fani.....11

2.2.0 Msuko.....12

2.2.1 Msuko mkuu.....13

2.2.2 Msuko kinzani.....14

2.2.3 Msuko msago.....14

2.2.4 Msuko kioo.....15

2.2.5 Msuko rudufu.....15

2.3.0 Muundo.....15

2.3.1 Muundo wa ki-vitushi.....16

2.3.2 Muundo wa ndani.....16

2.3.3 Muundo wa nje.....16

2.3.3.1 Beti.....16

2.3.3.2 Mishororo.....17

2.3.3.4 Mizani....18

2.3.3.5 Vina....18

2.3.3.6 Kibwagizo....19

2.4.0 Wahusika....20

2.4.1 Mhusika mkuu....21

2.4.2 Mhusika msaidizi....21

2.4.3 Mhusika bapa....21

2.4.4 Mhusika duara....22

2.5.0 Mandhari....22

2.6.0 Matumizi ya lugha....24

2.6.1 Maana na matumizi....24

2.6.2.0 Uhuru wa kishairi....27

2.6.2.1 Inkisari....28

2.6.2.2 Mazida....29

2.6.2.3 Tabdila....29

2.6.2.4 Ukiushi wa kisarufi....30

2.6.2.5 Ukiushi wa kimsamiati....30

2.6.2.6 Matumizi ya lahaja....31

2.6.2.7 Kiarabu....32

2.6.3.0 Tamathali za usemi....33

2.6.3.1 Tashibihi....34

2.6.3.2 Sitiari....34

2.6.3.3 Tashihisi / uhuishaji....35

2.6.3.4 Chuku....36

2.6.3.5 Maswali ya balagha....37

2.6.3.6 Nidaa....37

2.6.3.7 Methali....38

2.6.3.8 Takriri....38

2.6.3.9 Visawe....39

2.6.3.10 Misemo....39

2.6.3.11 Tanakali za sauti....39

2.6.3.12 Taashira / ishara....40

2.7 Hitimisho....40

## SURA YA TATU

## MSUKO NA MUUNDO KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*


3.0 Utangulizi ........................................ 41

3.1 Msuko katika *Utenzi wa Tambuka* ........................................ 41

3.2.0 Muundo katika *Utenzi wa Tambuka* ........................................ 46

3.2.1 Muundo wa nje ........................................ 47

3.3 Hitimisho ........................................ 49


## SURA YA NNE

## MANDHARI NA WAHUSIKA KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*


4.0 Utangulizi ........................................ 50

4.1.0 Mandhari katika *Utenzi wa Tambuka* ........................................ 50

4.2.0 Wahusika katika *Utenzi wa Tambuka* ........................................ 56

4.2.1.0 Wahusika wa Kiislamu ........................................ 57

4.2.1.1 Mtume Muhammadi ........................................ 57

4.2.1.2 Ali ........................................ 59

4.2.1.3 Mwenyezi Mungu ........................................ 60

4.2.1.4 Malaika Jibrili ........................................ 61

4.2.1.5 Mughera ....................................................61

4.2.1.6 Karari ....................................................62

4.2.1.7 Mkewe Ali ....................................................62

4.2.1.8 Wahusika wa kimakundi wa Kiislamu ....................................................63

4.2.2.0 Wahusika wa Kikristo ....................................................64

4.2.2.1 Mfalme Herekali ....................................................64

4.2.2.2 Askofu Waziri ....................................................65

4.2.2.3 Wahusika wa kimakundi wa Kikristo ....................................................65

4.2.3.0 Wahusika wanaobadilika ....................................................66

4.2.3.1 Jasusi ....................................................66

4.3 Hitimisho....................................................67

## SURA YA TANO

## MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

5.0 Utangulizi ....................................................68

5.1.0 Uhuru wa kishairi ....................................................68

5.1.1.0 Ukiushi wa kimofolojia ....................................................68

5.1.1.1 Inkisari ....68
5.1.1.2 Mazida ....69
5.1.1.3 Tabdila ....69
5.1.2.0 Ukiushi wa kimsamiati ....70
5.1.2.1 Lahaja ya Kingozi ....70
5.1.2.2 Lahaja ya Kiamu ....71
5.1.2.3 Kiarabu ....71
5.1.3.0 Ukiushi wa Kisintaksia ....73
5.2.0 Tamathali za usemi ....73
5.2.1 Tashibihi ....74
5.2.2 Sitiari ....75
5.2.3 Tashihisi ....77
5.2.4 Maswali ya balagha ....77
5.2.5 Methali ....78
5.2.6 Nidaa ....78
5.2.7 Takriri ....79
5.2.8 Chuku ....81
5.2.9 Visawe ....82

5.2.10 Misemo ....84

5.2.11 Ukinzani / Usambamba ....84

5.2.12 Tanakali za sauti ....85

5.2.12 Taashira ....86

5.3 Hitimisho ....88

## SURA YA SITA

## TATHMINI NA MAPENDEKEZO0

6.0 Utangulizi ....89

6.1 Muhtasari wa utafiti ....89

6.2 Kuhusu malengo ya utafiti ....91

6.3 Kuhusu nadharia tete ....92

6.4. Mapendekezo ya utafiti zaidi ....92

**Marejeleo** ....94

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 UTANGULIZI

Utenzi au utendi ni aina ya ushairi mkongwe sana unaojidhihihirisha kwa urefu wake. Pia hugusia maswala muhimu yanayomkumba binadamu katika shughuli za kila siku. Mojawapo ya maswala muhimu katika tenzi nyingi ni dini. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Fatuma*, tunamwona Mungu akimtuma Malaika Jibril kushughulikia na kutayarisha ndoa kati ya Ali na Fatuma.

Tumeshaona hapo awali kuwa tenzi hujipambanua kwa sifa zake maalum zilizo tofauti sana na mashairi ya kawaida. Ili kuthibitisha ukweli huu, tutaangalia fasili ya wataalamu kadha wa fasihi ya Kiswahili.

Mbatiah (2001) anasema kwamba, "utenzi ni aina ya ushairi unaojipambanua kwa urefu wake na uzito wa masuala unayoyashughulikia". Anaendelea kusema kuwa, "utenzi huwa ni mseto wa masimulizi na maelezo yenye urefu wa mamia au pengine maelfu ya beti kuhusu jambo fulani".

Wamitila (2003) anasema kuwa, "utendi hutumiwa kueleza shairi ndefu la kisimulizi linalozungumzia kwa mapana na mtindo wa hali ya juu ya matendo ya mashujaa au shujaa mmoja".

Kwa mujibu wa fasili hizi, tunaona kuwa tenzi nyingi zimejikita katika mtindo wa hadithi ndefu, inayohusu wahusika hasa mashujaa pamoja na matendo yao. Mbinu mbalimabili za lugha hutumika zinazotofautiana kutoka kwa mtunzi mmoja hadi mwingine.

*Utenzi wa Tambuka* ulitungwa mwaka wa 1728 na Bwana Mwengo bin Athumani huko Siu. Utenzi huu unahusu tukio la vita baina ya Waislamu na Wakristo huko Syria. Vita hivi vinaanzishwa na Waislamu kwa lengo la kulipiza kisasi kufuatia kuuawa kwa Jaafari, ambaye ni mmojawapo wa masahaba wa Mtume Muhammadi wakiwa mikononi mwa mfalme Herekali wa Tambuka. Vita hivi vinachukua muda mrefu na vinadhihirisha mapambano makali mno. Ingawa kila upande unajizatiti kwa nia ya kutwaa ushindi, Waislamu ndio wanaoibuka washindi. Mfalme Herekali anauawa na ufalme wake unaporomoka.

Tunatarajia ya kwamba *Utenzi wa Tambuka,* kama zilivyo tenzi zingine una mawazo mazito sana kuhusu vita vya kidini kati ya Warumu na Waarabu. Mawazo haya yamewasilishwa kwa kutumia fani mbalimbali. Ni muhimu kuchunguza na kuchanganua mbinu zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe katika utenzi huu. Bila kufanya hivyo, itakuwa vigumu kwa wasomaji wa fasihi kulinganisha na kulinganua fani katika tenzi za kale na mashairi ya kisasa.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo la utafiti huu ni kuhakiki vipengele vya fani katika *Utenzi wa Tambuka.* Fani hujumuisha vipengele muhimu ambavyo kwa pamoja, huipa kazi ya kifasihi umbo lake.

Aidha, vipengele vya fani vina uamili mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi kwa hadhira yake. Mbali na hayo, matumizi mazuri ya vipengele vya fani huifanya kazi ya kifasihi kuvutia hadhira lengwa. Kwa upande mwingine, kutomakinika kwa mtunzi katika matumizi ya fani huinyima kazi ya kifasihi umbo nzuri. Matokeo yake ni kuwa kazi ya kisanii hukosa mshikamano na mwingiliano unaotarajiwa. Matini ya aina hiyo huwa haina uwezo wa kuvutia hadhira.

Wahakiki ndio hupima kufana au kutofana kwa mwandishi katika utunzi wake. Fani huwa ni kigezo muhimu cha kupimia kufana au kutofana huko. Hata hivyo, hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu *Utenzi wa Tambuka* kifani. Kutokana na pengo hili, tumeona kuwa kuna haja ya kuuhakiki utenzi huu kifani. Utafiti wetu utatuwezesha kubaini mbinu mbalimbali za kuwasilisha ujumbe zilizotumiwa na msanii. Matarajio yetu ni kuwa utafiti huu utachangia pakubwa katika fasihi kwa jumla.

## 1.2 MALENGO YA UTAFITI

Malengo yetu makuu katika utafiti huu ni:

i) Kubainisha vipengele mbalimbali vya kifani vilivyotumika katika *Utenzi wa Tambuka.*

ii) Kutathmini kufana au kutofana kwa mtunzi katika matumizi ya fani katika *Utenzi wa Tambuka.*

iii) Kubainisha namna vipengele mbalimbali vya kifani vinavyoingiliana na kukamilishana katika ujenzi wa umbo moja la *Utenzi wa Tambuka.*

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Baada ya kudurusu tahakiki mbalimbali zilizofanywa kuhusu tenzi mbalimbali za Kiswahili, tuligundua kuwa hakuna uhakiki wowote wa kitaalamu uliofanywa kuhusu *Utenzi wa Tambuka* katika Kiswahili.

*Utenzi wa Tambuka*, sawa na tenzi nyingine za kale zimetungwa kwa msamiati wa kale ambao hautumiki kwa sasa. Aidha, tenzi zenyewe ni ndefu na zenye matumizi ya mseto wa lahaja kwa wingi. Hali hii imefanya wasomaji wengi kuhofia kuzisoma. Wasomaji wengi huenda wasipate ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi wa utenzi fulani kwa sababu ya uchangamano wa lugha.

Hali hii ndiyo imetupa changamoto ya kuhakiki *Utenzi wa Tambuka* ili kuwafaidi wasomi wa Kiswahili kwa kuwasahilishia uelewekaji wake. Pia, uhakiki wa utenzi huu utamwezesha msomi wa Kiswahili kulinganisha matumizi ya lugha ya Kiswahili ilivyo sasa na jinsi ilivyotumika katika enzi za kale.

Pamoja na hayo, tuliteua mada hii ili kutoa mchango wetu wa kiusomi katika ushairi wa Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, tunalengana kuwatia shauku wanafunzi kufurahia ushairi wa Kiswahili.

## 1.4 UPEO NA MIPAKA

Utafiti huu unahusu matumizi ya fani katika *Utenzi wa Tambuka*. Ili kufanikisha uhakiki huu tutatumia nadharia ya Umuundo, ambayo husisitiza kuwa uhakiki wa kifasihi ufanywe bila ya urejelezi wa nje. Kunga wanazozitumiua wasanii katika uwasilishaji wa ujumbe ndio lengo letu. Kwa kuwa dhana ya fani ni pana na ina vipengele vingi, tumechagua kuhakiki vitano, ambavyo ni ploti / msuko, muundo, mandhari, wahusika na mtindo (matumizi ya lugha). Tunajadili namna vipengele hivi vya kifani vilivyotumiwa, uamili wake wa kiumbuji na mchango wake katika muundo au umbo la kazi nzima.

Ni vigumu sana kutenganisha fani na maudhui kwa sababu fani ndiyo husitiri maudhui katika kazi yoyote ya kifasihi. Hivyo, tumegusia maudhui kwa namna yanavyoingiliana na fani katika *Utenzi wa Tambuka*. Lengo letu kuu ni kushughulikia fani na iwapo tutaangalia maudhui kwa undani, tutakuwa tumekiuka mipaka ya nadharia ya Umuundo.

Tumedurusu kazi mbalimbali za wasomi wengine ili kuelewa madai yao kuhusu fani. Tutasoma pia *Utenzi wa Tambuka* na kuuchanganua kifani.

## 1.5 NADHARIA TETE

Utafiti huu ulifanywa kwa misingi ya nadharia tete zifuatazo:

i) *Utenzi wa Tambuka* una ukwasi wa mbinu za kifani na unadhihirisha usanifu wa hali ya juu.

ii) Vipengele mbalimbali vya kifani katika *Utenzi wa Tambuka* vimechangia pakubwa

katika muundo wa umbo la utenzi wenyewe.

## 1.6 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Mengi yameandikwa kuhusu dhana ya fani katika fasihi ya Kiswahili. Vilevile, kuna tahakiki kadha zilizofanywa kuhusu fani katika matini mbalimbali za kifasihi za Kiswahili. Hata hivyo, sio mengi yaliyoandikwa kuhusu *Utenzi wa Tambuka*.

Knappert, J. (1979) amefanya utafiti mbalimbali kuhusu mashairi ya Kiswahili na historia yake katika karne ya kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa na ishirini. Katika harakati hizo, Knappert anatoa muhtasari wa utamaduni wa upwa wa Afrika mashariki na kuonyesha namna utamaduni huo ulivyoathiri kazi za kishairi zilizotungwa katika karne hizo.

Katika utafiti huu, Knappert ameelezea kuwa *Utenzi wa Tambuka* ulitungwa na Athumani bin Mwengo huko Siu katika mwaka wa 1728. Pia, anatoa muhtasari wa *Utenzi wa Tambuka*. Mambo haya yanayoelezwa na Knappert yanatusaidia kujua machache ya kimsingi kuhusu *Utenzi wa Tambuka*. Pia, yanatusaidia katika kupata muhtasari wa utenzi huu, ambao ni muhimu katika kuelezea msuko wake.

Vilevile, Knappert, J. (1967) ametafsiri beti chache za *Utenzi wa Tambuka* kwa Kiingereza. Pamoja na tafsiri hiyo, Knappert ameelezea kuhusu utunzi wa *Utenzi wa Tambuka* na kisa kinachohusika.

Ingawa kazi za Knappert zinatudokezea machache kuhusu *Utenzi wa Tambuka*, hazituelekezi moja kwa moja katika fani ya utenzi huu. Pia, maelezo hayo yanatolewa sio katika mtazamo wa kifasihi, bali katika mtazamo wa Kianthropolojia. Kinyume na uchunguzi wa Knappert, uchunguzi huu unachukua mtazamo wa kifasihi. Pia, uchunguzi wetu unawalenga wasomi wa fasihi ya Kiswahili na wala sio wageni aliowalenga Knappert.

Kama tulivyotaja mwanzoni, *Utenzi wa Tambuka* ni miongoni mwa tenzi ndefu na za zamani sana kuwahi kutungwa katika Kiswahili.Mara yangu ya kwanza kusikia kuhusu utenzi huu ilikuwa kupitia kwa mihadhara niliyohudhuria.Utenzi huu unahusu vita kati ya Wakristo na Waislamu.Kupitia kwa maelezo ya wahadhiri wangu pamoja na kusoma utenzi wenyewe nilipata shauku ya kuufanyia uhakiki kwa manufaa ya siku sijazo. Kutokuwepo kwa marejeleo muhimu kuhusu utenzi huu kunaashiria pengo katika uhakiki wa mashairi ya Kiswahili. Tunatarajia ya kwamba uhakiki huu utakuwa msingi wa marejeleo ya kifasihi kuhusu utenzi huu.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA YA UTAFITI

Uhakiki huu umejikita katika nadharia ya Umuundo. Nadharia hii itatufaa sana katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani katika *Utenzi wa Tambuka* ili kubainisha jinsi vipengele hivyo vinaungana na kuunda umbo la kazi nzima.

Earlich (1969) anaeleza kuwa nadharia ya Umuundo inahusishwa na wana-isimu wa shule ya Prague kati ya miaka ya 1928-1946, ambao walihusika na Urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Earlich (k.h.j) anaendelea kueleza kuwa kuzuka kwa Shule ya

Isimu ya Prague (SIP) kulihusishwa sana na Urasimu na hasa kikundi kimoja cha wana-isimu wa Moscow.

Miongoni mwa waasisi wa nadharia ya Umuundo ni Roman Jakobson, Jan Mukarovsky, N.S. Trubetzkoy, Boris Tomaserky na Ren Wellek. Culler, J. (1975:4) anaeleza kuwa wasomi hawa waliathiriwa na mawazo ya Ferdinand de Saussure kuhusu dhana za kiisimu za *Langue* na *Parole*.

Sausure alibaini kuwa 'Parole' ni lugha ya kimatumizi ilihali 'langue' ni mfumo lugha ulio na jumla ya taratibu za lugha ambazo kila msemaji wa lugha hizo anazifahamu. Kulingana na Saussure, 'langage' huundwa kwa 'langue' na 'parole'. Kwa kurejelea dhana hizi, wana Umuundo walielezea kuwa fasihi inaweza kuangaliwa kama mfumo wenye kanuni zake ambazo kila msanii wa fasihi anahitaji kuelewa na pia aelewe jinsi ambavyo mfumo huo unavyoweza kutumiwa katika mawasiliano na hata kimuundo.Walisisitiza kuwa ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, lazima mhakiki achunguze matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipashio vyake na mahusiano ya vipashio hivyo. Kwa mantiki hii, wanaumuundo walielekea kuashiria kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama *langue* kwa kuwa na kanuni zake. Hivyo, kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni za utanzu unaoitawala. Kwa mfano katika kuhakiki *Utenzi wa Tambuka*, tunastahili kuchanganua lugha ilivyotumiwa pamoja na kaida zinazotawala utunzi wa tenzi na kutathmini ikiwa mtunzi anatekeleza kaida hizo.

Pia, wanaumuundo walitumia dhana ya ukinzani uwiliuwili iliyobuniwa na Saussure. Walieleza kuwa dhana hii inaweza kutumiwa kuelezea maana ya maneno kutokana na vinyume vya maneno hayo. Ukinzani uwiliuwili katika fasihi unaweza kutumiwa katika vipengele zaidi kama vile kutofautisha sifa za wahusika.

Pia, wanaumuundo walitumia dhana za Saussure za kiashiria na kiashiriwa. Saussure aliuona ulimwengu wa lugha kuwa unaojengwa kwa viashiria na viashiriwa na kuwa viashiriwa hubainishwa na viashiria. Wanaumuundo walionelea kuwa vipengele mbalimbali vya fani ndivyo viashiria. Maana inayotokana na vipengele hivi ndivyo viashiriwa.

Wanaumuundo walijihusisha na uhakiki wa mashairi na tungo nyingine za kifasihi. Walichunguza upatanifu wa kisauti, vina, mizani, wizani, toni, na arudhi kwa jumla. Pia, walisisitiza umbo la msuko, hadithi na usawiri wa wahusika. Pia, wanaumuundo walisisitiza hali ya juu ya ubunifu katika matumizi ya lugha. Walipendekeza mbinu za ukiushi katika matumizi ya lugha kama vile tamathali za usemi.

Wanaumuundo walisisitiza uhuru na upekee wa kazi ya kifasihi. Waliamini kuwa kazi ya kisanaa haifai kuwa na urejelezi wa nje. Walipinga hatua ya kuihusisha fasihi na miktadha ya kijamii, kihistoria, kisiasa na kifilosofia.

Nadharia ya Umuundo inatufaa katika utafiti huu kwa kuwa inatilia mkazo muungano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya kifani katika ujenzi wa umbo moja la kazi ya kifasihi. Hivyo, inaafiki malengo yetu katika utafiti huu.

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu tumeufanya katika maktaba ambapo tumedurusu matini kadha zenye manufaa kwa utafiti wetu kama vile vitabu, tasnifu zilizojadili fani na pia majarida na makala mbalimbali yaliyo na mada zinazorejelea tenzi kwa jumla.

Kisha, tulisoma yale yaliyoandikwa juu ya *Utenzi wa Tambuka*. Pia, tulisoma utenzi wenyewe na kuuchanganua kifani. Tulitilia mkazo msuko, muundo, mandhari, wahusika na mtindo. Pia tulishauriana na wasomi na watalamu wengine wa fasihi hasa katika uwanja wa ushairi.

## 1.9 HITIMISHO

Sura hii imehusu mambo ambayo ni ya kiutangulizi ya utafiti huu. Imeelezea mambo kama vile utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada hii, mipaka na upeo, nadharia tete msingi wa kinadharia wa utafiti na njia za utafiti. Sura ifuatayo inahusu misingi ya uhakiki wa fani.

# SURA YA PILI

# MISINGI YA UHAKIKI WA FANI

## 2.0 UTANGULIZI

Sura ya kwanza imehusu mambo ya kiutangulizi ya utafiti huu. Sura hii ya pili inahusu ufafanuzi wa misingi ya uhakiki wa fani. Mwanzo kabisa, tunafafanua dhana ya fani na kueleza vipengele vyake mbalimbali. Kwa kuwa vipengele vya fani ni vingi na vipana mno, vipengele tunavyovielezea ni vile ambavyo tunavitumia katika utafiti huu. Vile vingine tunavitaja tu. Tunatoa mifano ya hapa na pale kutoka tenzi za Kiswahili.

## 2.1 DHANA YA FANI

Dhana ya fani katika fasihi ya Kiswahili imeelezwa na kufafanuliwa na waandishi mbalimbali. Miongoni mwa waandishi hawa ni Njogu na Chimera (1999), Mbatiah (2001) na Wamitila (2002, 2003).

Wamitila (2003) anaeleza kuwa fani hutumiwa kuelezea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Fani huelezea mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui.

Naye Mbatiah (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza, ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi

cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Pili, ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya .

Kwa uchunguzi wetu, tunaona ya kwamba wataalamu hawa wawili wanaelekea kukubaliana katika kijelezi cha kwanza kuwa fani ni vipengele vya kimtindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahsusi. Kijelezi hiki kina maana kuwa fani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa.

Kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu : Maudhui na fani. Maudhui huwa ni maana au ujumbe unaojitokeza katika kazi ya fasihi. Kwa upande mwingine, fani huwa ni jumla ya mbinu za kuwasilishia maudhui.

Kutokana na fafanuzi zinazotolewa na waandishi mbalimbali wa fasihi, ni wazi kuwa dhana ya fani ni pana na ina vipengele vingi. Miongoni mwa vipengele muhimu vya fani ni msuko / ploti, muundo, wahusika, mtindo, mandhari, usimulizi, toni / lahani, wakati n.k. Kwa kuwa vipengele hivi vya fani ni vingi, mhakiki anafaa kuchagua baadhi yavyo katika uhakiki wake. Vipengele anavyovichagua vitalingana na nia au madhumuni yake katika uhakiki huo. Katika utafiti huu, tumechagua kuhakiki vipengele vya msuko, muundo, mandhari, wahusika na mtindo. Vipengele hivi tunavifafanua hapa chini.

## 2.2.0 MSUKO

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Njogu na mwenzake

wanaendelea kueleza kuwa msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana.

Kwa ujumla, msuko hurejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na huhusisha matendo ya mhusika mkuu na jinsi yanavyowaathiri wahusika wengine katika kazi ya kifasihi. Kwa kawaida, msuko huelezea jinsi ambavyo matukio hufuatana kiusababishi. Ni lazima kuwepo na matarajio ambayo yanaongezea nguvu matukio fulani katika kazi ya kifasihi. Msuko pia hujulikana kama ploti.

Wamitila (2003) ameainisha misuko mbalimbali: msuko kinzani, msuko msago, msuko mkuu, msuko kioo na msuko rudufu.

### 2.2.1 Msuko mkuu

Msuko huu unahusu hadithi kuu katika kazi ya kifasihi. Msuko mkuu hupatikana pale ambapo kazi ya fasihi ina hadithi kadha ambazo kila moja ya hadithi hizo inatambulika. Kimsingi, msuko mkuu huhusisha matendo na maelezo kuhusu mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Mwana Fatuma,* msuko mkuu ni ule wa harusi ya Fatuma na Ali. Mtunzi wa utenzi anaranda hapa na pale badala ya kutuelezea kuhusu harusi yenyewe moja kwa moja. Anasimulia vijihadithi vingine kama vile sifa za Mtume Muhammadi, sifa nzuri za Fatuma, mauti ya Khadija na matayarisho ya ndoa huko mbinguni.

### 2.2.2 Msuko kinzani

Ni ploti inayoelezea matukio ambayo yanakusudia kufikia lengo tofauti na lile la msuko mkuu. Hoja hii ina maana kuwa msuko wa aina hii huhusishwa na mhusika anayepingana na mhusika mkuu. Mhusika wa aina hii atatenda matendo yanayoonyesha kupinga au kuasi matendo au mwelekeo unaochukuliwa na mhusika mkuu.

Katika hali hii, mhakiki anafaa aangalie malengo ya mhusika mkuu na yale ya mhusika anayepingana na mhusika huyo. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Siri li Asirali*, Anzaruni anakinzana na Ali lakini mwishowe anashindwa. Hivyo, matendo yote ya Anzaruni yanafaa kuchukuliwa kuwa msuko kinzani.

### 2.2.3 Msuko msago

Msuko msago hutumiwa kuelezea matukio yanayofuatana kwa njia ya moja kwa moja bila ya kuwa na matumizi ya mbinu rejeshi. Wamitila (2003:143) anaeleza kuwa matukio hufuatana kwa njia ya A-B-C-D n.k. Waandishi wengine huurejelea msuko wa aina hii kama msuko sahili.

Msuko wa aina hii unapatikana katika *Utenzi wa Ayub*. Katika utenzi huu, hali ya Ayub ya kumcha Mungu inasababisha Ibilisi kumuomba Mungu ruhusa amjaribu kwa mali na afya yake. Kuugua kwa Ayubu kwa muda mrefu kunasababisha Rehema atafute kazi kwa majirani ndiposa apate chakula. Kisha, Ibilisi anamletea Ayub majaribu mengine mengi yakifuatana. Hatimaye, tunaona Ayub akiibuka mshindi kwani anapona na kurudishiwa mali yake na Mungu. Msuko huu pia unapatikana katika *Utenzi wa Mwana*

*Munga* ambapo Fumo Liyongo anamsifu mpenzi wake kuanzia kichwani, usoni, shingoni, mabegani, kifuani, tumboni, nyongani, mapajani, magotini hadi miguuni.

### 2.2.4 Msuko kioo

Msuko kioo ni aina ya msuko ambao unaenda nyuma na mbele. Msuko wa aina hii huhusisha mbinu rejeshi kwa wingi. Msuko huu pia huitwa msuko changamano. Msuko wa aina hii umetumiwa sana katika utanzu wa riwaya changamano ya Kiswahili. Katika mashairi ya tenzi, hupatikana katika tenzi ndefu kama *Utenzi wa Rasi 'lGhuli.*

### 2.2.5 Msuko rudufu.

Msuko rudufu ni msuko ambao unahusisha zaidi ya msuko mmoja katika kazi ya kifasihi. Misuko inayopatikana katika kazi ya aina hiyo inafaa kuwa na nafasi sawa.Yaani hadithi mbalimbali zinazopatikana katika kazi hiyo zinaweza kujisimamia na kila moja ikatambuliwa waziwazi.

## 2.3.0 MUUNDO

Muundo ni umbo la kitu. Muundo unaelezea jinsi kitu fulani kilivyoundwa kwa kukitazama na hata kukigusa. Muundo pia hurejelea jumla ya uhusiano unaokuwako kati ya visehemu mbalilmbali vinavyounda kitu kamili au cha kijumla. Katika utafiti wetu tutaangalia muundo kama vile vijisehemu vidogovidogo ambavyo huunda kazi nzima ya kifasihi.

Wamitila (2003:153) anasema kuwa muundo unaweza kuwa wa ki-vitushi, muundo wa ndani ama muundo wa nje.

### 2.3.1 Muundo wa ki-vitushi

Hutumiwa kuielezea kazi ya kinathari ambayo inajumlisha hadithi au vihadithi vinavyoelekea kujitegemea lakini vina kiunganishi fulani kinachoviunganisha. Kimsingi, muundo katika mtazamo huu unaingiliana na dhana ya msuko. Kigezo kinachotumiwa ni cha hadithi au visa.

### 2.3. 2 Muundo wa ndani

Hii ni dhana inayotumika kuelezea sifa za ndani za kazi ya kifasihi. Kwa mfano, jinsi sehemu mbalimbali zinavyohusiana kama wahusika na mandhari, mtazamo na mandhari na wahusika na matumizi ya lugha. Kwa mfano katika utenzi wa Ayubu Ibilisi anahusiana na Mungu kumjaribu Ayubu.

### 2.3.3 Muundo wa nje

Muundo wa nje hutumiwa kuelezea wasifu wa nje wa kazi ya kifasihi. Muundo huu unahusiana na urefu, mgawo, sura au maonyesho ya kimpangilio. Kwa mfano, katika ushairi muundo wa nje utahusu idadi ya beti, idadi ya mishororo, idadi ya mizani mtiririko wa vina n.k. Kwa jumla ni jinsi shairi fulani linavyoonekana kwa nje.

#### 2.3.3.1 Beti

Ni kifungu cha mishororo katika ushairi. Hakuna idadi ya beti inayokubaliwa kila shairi kuwa nayo. Kuna baadhi ya mashairi ambayo yana beti nyingi sana ilhali mengine huwa na beti chache. Tenzi zinajulikana kuwa na beti nyingi. Kwa mfano, *Utenzi wa Rasi*

*'lGhuli* ambao unacjulikana kuwa mrefu zaidi katika Kiswahili una beti elfu nne mia tano.

### 2.3.3.2 Mishororo

Mshororo ni msitari wa ubeti wa shairi. Idadi ya mishororo ni mojawapo wa vigezo vya kuainisha mashairi katika aina mbalimbali. Kwa kawaida, shairi la aina ya tarbia huwa na mishororo minne katika kila ubeti. Nalo shairi la aina ya tathlitha huwa na mishororo mitatu katika kila ubeti. Tenzi huwa na mishororo minne katika kila ubeti. Hivyo, tenzi ni aina ya mashairi ya tarbia. Ufuatao ni mfano wa ubeti wa kwanza wa *Utenzi wa Mwana Kupona*.

**Negema wangu binti,**
**mchachefu hasanati,**
**upulike wasiati,**
**asaa ukazingatiya.**

Ubeti huu una mishororo minne.

### 2.3.3.3 Vipande

Vipande ni sehemu ya mshororo. Mishororo ya mashairi huweza kugawika katika sehemu au vipande mbalimbali. Kuna mashairi ambayo huwa yamegawika katika vipande viwili, yaani ukwapi na utao. Kwa mfano:

**Mhariri wa ujuzi, mwinyi siwe na hamaki,**

**Nimewanza wapinzi, kuwaza huwadiriki,**

**Japo waambiwa wazi, hudai hawashindiki.**

Mashairi mengine huwa yamegawika katika vipande vitatu: ukwapi, utao na mleo. Mishororo ya tenzi huwa ni kipande kimoja tu.

### 2.3.3.4 Mizani

Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo wa shairi. Idadi ya mizani huwa mojawapo wa vigezo vya kuainisha mashairi katika makundi au aina mbalimbali. Katika ubeti ufuatao, msanii ameweka mizani kumi na sita katika kila mshororo.

**M-ha-ri-ri- wa- u – ju - zi-, mwi – nyi- si – we – na – ha – ma – ki**
1 - 2-3- 4 5- 6- 7- 8, 9- 10- 11- 12- 13- 14- 15- 16

**Ni- me- wa- nza- wa- pi- nzi, ku- wa- za- hu- wa- di- ri- ki- i**
1- 2- 3- 4- 5- 6- 7 8- 9- 10- 11- 12- 13- 14- 15 – 16

**Ja- po- wa- a- mbi-wa wa- zi, hu- da- i ha- wa- shi- ndi- ki.**
1- 2- 3- 4- 5- 6 7- 8 9- 10- 11 12- 13- 14- 15- 16

### 2.3.3.5 Vina

Vina ni silabi za sauti namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadha katikati na mwisho wa kila mshororo katika ubeti wa shairi. Mfano ufuatao utatufafanulia zaidi vina

Mhariri wa uju**zi**, mwinyi siwe na hama**ki**,

Nimewanza wapin**zi**, kuwaza huwadiri**ki**,

Japo waambiwa wa**zi**, hudai hawashindi**ki**.

Katika ubeti huu, vina vya kati ni '**zi**' na vya mwisho ni '**ki**'

### 2.3.3.6 Kibwagizo

Ni maneno yaliyoko katika mstari wa mwisho wa ubeti wa shairi na ambayo hurudiwarudiwa katika kila mwisho wa ubeti. Katika beti zifuatazo, kibwagizo ni 'usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi'.

Dunia mti mkavu, kiumbe siumbile,

Ukaufanyia nguvu, hadhabati kwa ndole,

Mtiwa mtakavu, mara ulikwangushile,

**Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi**

Dunia mti mkavu, kiumbe siumbile,

Ukaufanya nguvu, hadhabati kwa ndole,

Mtiwa mtakavu, mara ulikwangusile,

**Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi**

Kibwagizo huwa na uamilifu wa kubeba ujumbe au maana mahususi inayopatikana katika shairi husika. Kwa hivyo, kibwagizo huwa na jukumu muhimu la kufasiria dhamira ya shairi hilo.

## 2.4.0 WAHUSIKA.

Wahusika ni viumbe tunaokutana nao katika kazi ya kifasihi na ambao kutokana na matendo na mazungumzo yao, wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.

Wahusika ni vijenzi muhimu vya tanzu za drama, riwaya, novela na hadithi fupi. Katika fasihi simulizi na fasihi andishi isiyo ya kiuhalisia, wahusika wanaweza kuwa wanyama wadudu, ndege, mazimwi au viumbe wengineo. Mbatiah (2001) amebainisha wahusika katika makundi matano makuu: mhusika bapa, mhusika duara, mhusika dufu, mhusika mkuu na mhusika msaidizi.

Naye Wamitila (2003) anasema kuwa mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wasifu wa mhusika unategemea mkabala uliopo katika kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kiuhalisia. Kazi hizi zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida.

Wamitila (k.h.j) ameainisha wahusika katika makundi kumi na sita : wahusika akisi, wahusika bapa, wahusika bapa sugu, wahusika bapa kielezo, wahusika batili, wahusika duara, wahusika ghibu, wahusika jumui, wahusika kipokeo, wahusika kani, wahusika wachomozi, wahusika wadogo / wasaidizi, wahusika wafoili, wahusika wakuu, wahusika wasimulizi na wahusika shinda. Katika sehemu hii, hatutaweza kuelezea aina hizi zote za wahusika. Tutaelezea tu aina chache ambazo zitatufaa katika utafiti huu.

### 2.4.1 Mhusika mkuu.

Mhusika mkuu ni mhusika ambaye huwa kiini cha kazi fulani ya kifasihi. Mhusika mkuu huitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Masimulizi yote humhusu yeye. Mhusika wa aina hii huwa nguzo muhimu ya kuyawasilisha maudhui na dhamira ya kazi husika. Kazi fupi na ndefu za kifasihi huwa na wahusika wakuu zaidi ya mmoja. Kazi fupi kama vile hadithi fupi huweza kuwa na mhusika mkuu mmoja au wawili. Mhusika mkuu hukuzwa kwa upana. Msuko mkuu humhusu yeye. Katika *Utenzi wa Ayub*, wahusika wakuu ni Ayub na Ibilisi

### 2.4.2 Mhusika msaidizi

Mhusika msaidizi ni mhusika ambaye husaidia mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi. Pia hujulikana kama mhusika mdogo. Mhusika wa aina hii hachukui nafasi kubwa kama mhusika mkuu bali hutokeza hapa na pale. Mhusika msaidizi hutumiwa kusaidia katika ujenzi wa maudhui na sifa za mhusika mkuu. Wahusika wasaidizi huweza kuwa wengi. Wahusika hawa huwa hawakuzwi sana. Huweza kutokea na hata kupotea kabisa hata wasionekane tena. Katika *Utenzi wa Ayub*, wahusika wasaidizi ni pamoja na Mungu, Rehema, na Malaika Jibrili.

### 2.4.3 Mhusika bapa.

Mhusika bapa ni aina ya mhusika ambaye habadilikibadiliki katika kazi ya kifasihi. Mhusika wa aina hii huwa na sifa na matendo yaleyale kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ikiwa ana sifa mbaya, sifa hizo huendelea hadi mwisho wa kazi ya kifasihi. Ikiwa ana

sifa nzuri, sifa hizo pia huendelea hadi mwisho. Wahusika bapa wanaweza kugawanywa katika makundi mawili. Wahusika bapa kielelezo na wahusika bapa sugu.

Mhusika bapa sugu ni mhusika ambaye anachukua msimamo fulani madhubuti au sugu katika kazi ya kifasihi. Mhusika huyo hujulikana au kutambulika kutokana na msimamo huo wake ambao unaweza kuwa mzuri au mbaya. Kwa upande mwingine, mhusika bapa kielelezo huwa hana msimamo fulani sugu lakini habadiliki kitabia. Katika *Utenzi wa Ayub*, Ibilisi anaweza kuwa mfano wa mhusika bapa sugu. Kwa upande mwingine, mhusika bapa kielelezo huwa na sifa au tabia nzuri ambazo huchukuliwa kuwa kielelezo au kitu cha kuigwa. Rehema katika *Utenzi wa Ayub* ni mfano mzuri wa mhusika wa aina hii. Rehema ana sifa ya mhusika mvumilivu, mwenye bidii na vilevile mcha Mungu.

### 2.4.4 Mhusika duara.

Mhusika duara ni kinyume cha mhusika bapa. Mhusika duara hubadilikabadilika kitabia kila mara. Kutokana na kubadilika kwakwe, mhusika duara huonekana kuwa na sifa zinazokaribiana na zile za binadamu wa kawaida. Kubadilika kwake pia huwa ni njia ya kuonyesha uhalisia wa kijamii.

## 2.5.0 MANDHARI

Wamitila (k.h.j) anasema kuwa mandhari ni dhana ambayo hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia. Ni mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Katika maana

pana, dhana hii huelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa fasihi.

Mbatiah (2001) anasema kuwa istilahi hii inahusiana hasa na utanzu wa drama. Inarejelea sura mahususi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yaliyoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mbatiah anaendelea kusema kuwa mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Istilahi ya mandhari pia hutumiwa kwa maana ya sura ya mahali, hasa ikiwa inavutia.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, tunaweza kueleza mandhari kama mazingira ya kimahali na wakati wa kihistoria ambamo kazi fulani ya kifasihi hujikita. Kila kazi ya kifasihi, iwe tamthilia, ushairi, riwaya, hadithi fupi au novela huwa na mandhari yake.

Msanii anaweza kuchagua mandhari yake kulingana na ujumbe wake kwa hadhira. Tukichukulia mfano kuwa, iwapo msanii ananuia kupasha ujumbe wa kuzorota kwa uchumi, tutaona kuwa mandhari yake yatakuwa yenye nyumba zisizopendeza, watu waliodhoofika, michoro ambayo shamba ni finyu, hamna bustani na hata wenyeji wanaonekana wakiwa na matambara na wenye huzuni. Mandhari haya hayapendezi wala kuvutia hata kidogo lakini bado ni mandhari yenye lengo maalum.

Kipengele cha mazingira kimegawika katika migao mitatu:

i) Eneo halisi la kijiografia au maelezo ya jinsi chumba, sehemu au mahali fulani palivyo.

ii) Amali za wahusika na desturi za maisha yao ya kila siku.

iii) Wakati ambapo tukio fulani linatendeka, ama kipindi maalum cha kihistoria au kipindi cha mwaka.

Mandhari hutumiwa na msanii ili kutekeleza majukumu fulani kando na kule kufichua tendo fulani lilitendeka wapi na lini. Msanii anaweza kutumia mandhari kama kielezi ambapo anatoa maelezo kuhusu tukio au matukio fulani yanapotendeka. Yeye hufanya hivi ili kuupatia utunzi wake mwelekeo ufaao na pia kumulika matukio mengine katika hadithi.

Msanii pia hutumia mandhari kuwasawiri wahusika wake kifasihi. Namna ambavyo huathiriana ndivyo mandhari yanavyoweza kumwathiri mhusika. Katika hali halisi, tunaona kuwa mandhari aishimo mtu humfanya awe na hulka aliyonayo. Katika usawiri wa mhusika kwa kutumia mandhari, mhakiki wa kazi za kifasihi anafaa aisome hadithi nzima na kuona jinsi ambavyo mhusika anavyobadilika kufuatia kule kubadilika kwa mandhari.

Kwa ujumla, tunaona kuwa mandhari yanahusu wakati na mahali ambapo kazi ya kifasihi inatendeka. Mandhari huweza kuibua hisia tofautitofauti kwa hadhira.

## 2.6.0 MATUMIZI YA LUGHA

### 2.6.1 Maana na matumizi

Lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambao hutumiwa na watu au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana. Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa lugha

yoyote ile hutumiwa kwa urahisi wa kustaajabisha na wazaliwa wa lugha fulani wanapokutana na kuzungumza kwa kutumia lugha fulani na kuelezeana habari za aina mbalimbali. Kupitia kwa maelezo ya Habwe na mwenzake, tunapata kufahamu kuwa dhima kuu ya lugha ni mawasiliano.

Kamusi ya Kiswahili sanifu (2004) inasema kuwa lugha ni mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana ambayo hutumiwa na watu wa taifa au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana.

Naye Mgullu (1999) akimnukuu Sapir (1921) anasema kuwa lugha ni mfumo ambao mwanadamu hujifunza ili autumie kuwasilisha mawazo, maono na mahitaji. Mfumo huu hutumia ishara ambazo hutokea kwa hiari.

Kutokana na mawazo na maelezo ya wataalamu hawa, tunaona kuwa lugha hutumiwa na wanadamu na imekuwa ikitumiwa hivyo tangu jadi. Tofauti na lugha ya kawaida itumiwayo na wanajamii, taaluma ya fasihi imeweza kupata lugha yake tambulishi ambayo hutofautiana kwa kiasi fulani na lugha ya kawaida au ya taaluma nyinginezo

Wamitila (2003) anakubaliana na mawazo hayo na kusisitiza kuwa lugha ndiyo nyenzo inayotofautisha fasihi na sanaa nyingine kama uchoraji, ufinyanzi na nyinginezo. Tukiangalia fasili hizo zote, jambo kuu ni ule uamilifu wa lugha kama chombo cha kupasha habari. Lugha yaweza kuwa ya mazungumzo, ya maandishi au ya ishara lakini kwa jumla mawasiliano hupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Pia tunaona

ya kwamba sauti hizi za lugha zitumiwazo kwa mawasiliano ni zao la jamii na wala si la mtu binafsi.

Katika uhakiki wa kazi ya kifasihi, mhakiki hawezi kukwepa suala la lugha kwa maana hiyo ndiyo nyenzo kuu ya fasihi.

Katika sehemu hii tutabainisha sifa za lugha ya kishairi pamoja na dhima yake na jinsi inavyojipambanua na lugha ya kawaida. Katika kazi nyingi za kifasihi, tunaona kuwa wasanii hufuata utaratibu fulani wanapotunga kazi za kifasihi. Hata hivyo, kuna wakati ambapo wanaweza kuiboronga lugha na kukiuka kaida za lugha hiyo mno. Jambo hili hufanywa na msanii kutimiza lengo fulani. Pengine anataka kuonyesha upungufu alio nao mhusika fulani au pengine jinsi mhusika fulani alivyo na tajriba fulani.

Sote tunafahamu kuwa lugha ya kishairi ni tofauti sana na lugha ya matumizi ya kawaida. Hii ni kwa sababu ya ule uhuru alio nao mshairi wa kutumia lugha apendavyo. Malenga ana uhuru wa kutumia lugha kwa kukiuka sarufi iliyoko. Anaweza kukiuka sarufi kisintaksia, kimofolojia na hata kisemantiki. Mshairi anaweza kuumbua maneno na kuyaumba upya hata kubadilisha maana na mpangilio wa maneno hayo.

Lugha ikitumiwa kwa namna ya kuvutia ndio huweza kunasa hadhira ambayo hufurahia kuisoma kazi fulani ya kifasihi. Ni vyema msanii aielewe hadhira yake ndiposa achague ni kiwango kipi cha msamiati atakachotumia. Msanii anaweza kuwa na mawazo mazuri ya kupasha hadhira yake lakini atumie lugha ngumu yenye msamiati mzito kiasi

kwamba hadhira lengwa isielewe hivyo basi kutofanikiwa katika malengo yake. Lugha ina jukumu kuu la kuwasilisha fikra ya msanii.

Tutaangalia viwango mbalimbali vya lugha katika uhakiki wetu ili kuona jinsi ambavyo lugha ni muhimu katika kazi za kifasihi. Tutazingatia viwango viwili vikuu: kiwango cha uhuru wa kishairi na kiwango cha tamathali za usemi.

### 2.6.2.0 UHURU WA KISHAIRI

Mbatiah (2001) anasema kuwa uhuru wa kishairi ni dhana iliyo na maana mbili zinazohusiana. Kwanza, ni uhuru wa mshairi kukiuka kaida na kanuni za matumizi ya lugha katika viwango vya msamiati, sarufi na sintaksia. Pili, ni uhuru wa mwandishi wa utanzu wowote kukiuka sio tu kaida na kanuni za lugha, bali pia kaida za kijamii na kweli za kihistoria. Mbatiah anaendelea kueleza kuwa ukiushi kama ule wa tamthilia ya Kinjeketile ambapo msanii anasema Kinjeketile wa historia ni binadamu na Kinjeketile wa mchezo ni kiumbe cha sanaa, hufanywa kimaksudi na waandishi ili kukidhi mahitaji ya kisanaa na kuleta athari mahususi za kifani na kimaana. Katika ushairi, kuna Fumo Liyongo ambaye ni kiumbe wa kisanaa. Kunaye pia jagina wa Wagala ambaye ni binadamu aliyeishi duniani. Alikuwa mwenye urefu usio wa kawaida na nguvu za ajabu. Mhakiki wa kishairi anafaa kutathmini kazi ya kifasihi kwa kuangalia ni vipi msanii amefaulu kuleta athari iliyonuiwa.

Kwa hivyo tunaona hoja ya kwanza ya Mbatiah (k.h.j) itatufaa sana katika uhakiki wa utenzi husika kwani tutathibitisha ni vipi mshairi ameweza kuiboronga sarufi yake na ni

kwa nia gani. Mshairi pia ana ule uhuru wa kutumia msamiati wa lahaja mbalimbali. Hali hii haimaanishi kuwa msanii ana uhuru wa kishairi pekee bali pia ana uhuru wa kutumia lugha kwa ujumla wake. Iwapo kazi yake itasomwa na msomi wa kawaida, anaweza kuuchukulia uhuru huu kama upungufu wa kuimudu lugha lakini kwa msomi wa fasihi atafahamu ule uhuru alio nao mshairi.

Katika kiwango hiki, tutaweza kuchunguza ni vipi msanii amefaulu katika matumizi ya uhuru wake ili kufikia malengo yake ya kisanii.

#### 2.6.2.1 Inkisari

Inkisari ni ukiushi katika kiwango cha kimofolojia ambapo mtunzi anafupisha baadhi ya maneno kwa kudondoa herufi kadhaa ili kupata idadi ya mizani au vina. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, tunapata inkisari katika ubeti wa 224 kama ifuatavyo:

> **Make** Liyongo hakika,
> Matanga aliyaweka,
> Watu wakasikitika,
> Kwa Liyongo kufia.

Katika ubeti huu, maneno mawili ‘mama yake’ yanafupishwa na kuwa ‘make’. Sababu ya kufanya hivi ni kuwa malenga anataka kutosheleza idadi ya mizani katika mshororo

huo. Iwapo angetumia 'mama yake', mshororo huo ungekuwa na mizani kumi na miwili kinyume na mizani minane kama ilivyo katika mishororo ya pili, tatu na nne.

#### 2.6.2.2 Mazida.

Mazida ni mbinu inayotumiwa katika utunzi wa mashairi kuongezea mizani ili kurefusha mishororo kwa madhumuni ya kusawazisha mizani ya mishororo katika ubeti Mazida ni ukiushi wa kimofolojia. Mfano wa mazida unajitokeza katika *Utenzi wa Fatuma* ubeti wa 405.

La ilaha ila ilahu,

Muhamadi **Rasuluhu.**

Katika mshororo wa pili wa ubeti huu, 'Rasua' limeendelezwa kama 'Rasuluhu'. Sababu ya kufanya hivi ni kuongeza idadi ya mizani ili kutosheleza idadi ya mizani katika mshororo huo na vilevile kupata urari wa vina.

#### 2.6.2.3 Tabdila

Tabdila ni mbinu inayotumiwa hasa katika ushairi kuirejelea ile hali ya kubadilisha maendelezo ya maneno fulani. Kimsingi, kutokana na sababu za kiarudhi ili kupata urari wa vina na kuongeza mvuto kwenye lugha. Mfano wa mbinu ya tabdila unapatikana katika *Utenzi wa Mwana Fatuma* ubeti wa 160;

Akamwambia: kanadi, kwa malaika junudi,

**Wangi** mno waso ahadi, uwasikiliza Makaa.

Katika ubeti ulionukuliwa hapo juu, 'wangi' limetumiwa kwa maana ya 'wengi'. Kwa hali hii, hijai yake imebadilishwa.

#### 2.6.2.4 Ukiushi wa kisarufi

Ukiushi wa kisarufi hujitokeza katika mahali ambapo maneno katika sentensi yanatokea katika mpangilio au mfuatano ulio kinyume au tofauti na ule wa kawaida. Kila lugha huwa na utaratibu wake wa kupanga maneno katika sentensi, vishazi na virai. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili hupendelea mfuatano wa nomino ikifuatwa na kivumishi, kitenzi na hatimaye kielezi. Katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani*, mbinu ya mpinduo sarufi inatokea kwingi kama vile katika ubeti wa 31:

**Hii ndio mama hali.**

Katika sarufi ya Kiswahili, mshororo huu ungetokea kama 'hii ndio hali mama'. Sababu ya kuiboronga sarufi kwa namna hii ni kuifanya lugha ya utunzi wa ushairi huu kuwa ya kuvutia zaidi. Pia, huwa ni njia ya watunzi kuonyesha umahiri wao wa kumudu miundo tofauti ya lugha husika.

#### 2.6.2.5 Ukiushi wa kimsamiati

Ukiushi wa kimsamiati hujitokeza katika ushairi kwa namna mbili. Kiwango cha kwanza kinahusu matumizi ya maneno ya kale. Maneno hayo ya kale huwa hayatumiwi tena katika lugha ya kawaida na matumizi yake huwa yamesalia tu katika ushairi.

Mifano ya maneno ya aina hii katika tenzi za Kiswahili ni 'Mukhuluku' (Mungu), 'Ngeu' (damu) n.k.

Baadhi ya maneno huweza kuendelezwa kwa namna isiyokuwa ya kawaida kwa sababu ya vina na mizani. Mifano:

Alifu (elfu)

Launi (mlaaniwa)

Nabiyaka (nabii)

### 2.6.2.6 Matumizi ya lahaja.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi. Washairi wana mazoea ya kutumia misamiati kutoka kwa lahaja mbalimbali katika utunzi wao. Matumizi ya maneno ya kilahaja huwa mojawapo wa uhuru wa matumizi lugha katika kiwango cha kimofolojia.

#### 2.6.2.6.0 Msamiati wa Kingozi.

Kingozi kinaaminika kuwa na asili yake katika mji wa kale sana ulioitwa Ngozi. Lugha yenyewe inajulikana kama Kingozi. Ni lugha ya zamani sana ya Pwani na miundo yake hupatikana tu katika ushairi lakini lugha yenyewe imepotea.

Badhi ya maneno ya Kingozi ni:

jitendele (jitendee),

akapulika (akasikia),

undetee (uniletee)

#### 2.6.2.6.1 Kiamu

Kiamu ni lahaja ya kale sana na ambayo inatumika mjini Amu na inajulikana pia kama Lamu. Jina Lamu lilitokana na kabila moja la Kiarabu ijulikanayo kama Banu Lami iliyotoka Ghuba la Uajemi. Jina la kale sana la Lamu lilikuwa 'Kiwa Ndeo'. Ni lugha iliyotumika sana Lamu, na imetumiwa sana katika uandishi wa tenzi za kale. Katika Kiamu, sauti /z/ hutumika badala ya /v/. /s/ hutumika badala ya /h/ na /j/ badala ya /y/.

Irabu /ee/ zikifuatana, konsonanti /l/ huwekwa kati. Kwa mfano,

**Makee** hubadilika na kuwa 'makelele'. **Mbee** hubadilika na kuwa 'mbele'

**Nyee** hubadilika na kuwa 'nyele'.

Katika Kiamu vilevile, konsonanti / l / na / r / hudondoshwa zikiwa katikati ya irabu mbili. Mfano:

**Chua** (chura), **kuea** (kulea), **kueta** (kuleta), **ngue** (nguruwe), **kutungi** (kutungulia).

### 2.6.2.7 Kiarabu.

Waarabu walikuwa baadhi ya wageni waliotembelea Pwani ya Afrika ya Mashariki. Walikuwa na lengo la kufanya biashara na pia kusambaza dini ya Kiislamu. Jambo hili lilisababisha maingiliano ya msamiati wa watu wa Pwani ya Afrika Mashariki kilugha. Matokeo yake ni kwamba lugha ya Kiswahili ilipata kukopa maneno mengi kutoka kwa

Kiarabu. Katika *Utenzi wa Ayub*, baadhi ya maneno ya Kiarabu yametumika kama vile katika ubeti wa kwanza:

Qalamu (kalamu).

Kukutubu (kuandika).

### 2.6.3.0 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi hujulikana pia kama lugha ya kitamathali. Ni ukiushi wa kimaksudi wa matumizi ya lugha. Tamathali za usemi hutumiwa kueleza fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi na kuwa na maana nyingine. Jambo hili linamaanisha kwamba tamathali za usemi hukiuka matumizi ya lugha katika viwango viwili yaani, kiwango cha kisemantiki na kile cha kisintaksia ili kuzua maana mpya au msisitizo.

Kuhenga (1977) katika dibaji ya kitabu chake anadai kuwa tamathali za usemi ni nguzo za ufasaha na pambo za lugha, na huwezesha mdarisi wa lugha kupakua baadhi ya uhondo uliofichika katika lugha. Madai haya ya Kuhenga yana maana kuwa tamathali za usemi ni mojawapo ya mbinu za kiubunifu za matumizi ya lugha kifasihi.

Ni vyema tufahamu ya kwamba, tamathali za usemi nyingi huwa na mpaka mdogo sana kati yazo. Msomaji anastahili kuwa na uelewa wa kina ili aweze kupata ujumbe ulionuiwa na mtunzi. Baadhi ya tamathali zinazotumika katika fasihi ya Kiswahili ni kama vile tashibihi, chuku, sitiari, tashihisi, visawe, takriri, nidaa, maswali ya balagha, misemo, kejeli, dhihaka, n.k. Katika sehemu hii, tutaelezea misingi ya uhakiki ya baadhi

ya tamathali za usemi. Tamathali tunazozijadili ni zile zilizotumika kwa kiwango cha juu katika *Utenzi wa Tambuka*.

### 2.6.3.1 Tashbihi

Tashibiha ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Vitu hivyo vinalinganishwa kwa kutumia viungo vifuatavyo: 'kama', 'mithili ya', 'fanana na', 'lingana na', 'ja', 'kama vile', 'sawa na', 'tamthili ya' n.k. Mbinu hii inapotumika, msomaji huweza kuichora taswira akilini mwake, jambo ambalo linarahisisha uelewekaji wa ujumbe. Ulinganisho huu ni wa moja kwa moja. Katika hali hii, kile kinacholinganishwa kinafahamika na msomaji.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, ubeti wa 327, Fatuma analinganishwa na mwezi. Tutathibitisha katika ubeti ufuatao:

**Akiwaa mmaizi,**
**binti ya Muombezi,**
**kama misali ya mwezi,**
**wa arbata ashari.**

### 2.6.3.2 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ielezayo sifa za kitu fulani kwa kusema kuwa ni ya kingine. Mbinu hii ya ulinganishi ni kama tashbihi isipokuwa hapana matumizi ya viungo. Ulinganishi huu huwa wa moja kwa moja.

Sitiari hutumika kwa nia ya kulenga hisia za msomaji na pia kujenga picha fulani akilini mwa binadamu ambaye ni msomaji wa kazi ya kifasihi inayohusika. Sitiari humwezesha msomaji kutafakari kuhusu taswira iliyojengeka akilini na kupata ufahamu wa kina wa wazo ambalo msanii ananuia kupasha hadhira yake. Kwa mfano:

Katika methali "ujana ni moshi, ukenda haurudi", 'ujana' unaitwa 'moshi'. Maana inayojitokeza katika methali hii ni ile ya kuonyesha kuwa ujana unapita na kuwa hautakuweko daima wala hauwezi kuzuiliwa usitoweke namna moshi usioweza kuzuiliwa.

Katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*, sitiari inadhihirika katika ubeti wa 99 ambapo Fatuma anaitwa nyota, ili kuashiria uzuri na urembo wake uangazavyo kila mahali. Ubeti wenyewe ni kama ifuatavyo:

**Endapo alikimwita,**
**'niilia, ewe Nyota !'**
**Fatuma akayivuta,**
**mbeleye akamwemea.**

### 2.6.3.3 Tashihisi / uhuishaji

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambapo vitu visivyokuwa na uhai husawiriwa kwa namna ilivyo sawa na binadamu ya kuweza kufikiri na kutenda. Tashihisi ni tamathali

ambayo hutumika ili kugusa hisia za msomaji au hata msikilizaji iwapo imetumika katika masimulizi.

wa Mutiso (2005) anasema kwamba asili ya tashihisi ni Kiarabu na maana yake ni kufanya kitu kiwe na maumbile au tabia ya nafsi ya mwanadamu.

Katika *Utenzi wa Mwana Kukua,* kuna tashhisi kadha. Mfano unapatikana katika ubeti wa 30 ambapo tunaelezwa kwamba 'roho' huona makubwa. Katika mfano huu, 'roho' imesimamia mwanadamu. Pia katika ubeti wa 891, tunaelezwa kwamba 'shingo' yake ilibeba. Shingo vilevile imetumiwa kusimamia mwanadamu.

### 2.6.3.4 Chuku

Chuku ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukipa kitu, mtu au hali kupita kiasi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusisitiza sifa hiyo ya ukubwa au udogo. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusisitiza na pia kuchekesha. Hali ambayo inamtia msomaji motisha ya kuendelea kuisoma kazi fulani. Katika utenzi wa *Siri Li Asirali* tunapata chuku katika ubeti 245.

**Kula mumoya rijali,**

**Kwemea mwende hajali,**

**Kukazuka zilizali,**

**Ba'azi yao ba'azi.**

Ubeti huu unasimulia vita kati ya Shekhe Ali na Anzaruni. Mtunzi anatujulisha kuwa kulitokea zilizali. Tunafahamu kuwa katika maisha halisi hatuwezi kuwa na mtetemeko wa ardhi kwa sababu ya vita vya watu wawili. Anachotufahamisha ni kwamba, vita hivyo vilikuwa vikali sana.

#### 2.6.3.5 Maswali ya balagha

Maswali ya balagha ni yale yanayoulizwa na msanii ili kumfanya msomaji awe macho lakini hayahitaji majibu. Mtunzi ametumia maswali ya balagha kwa kiasi katika utenzi huu kwa lengo la kumfanya msomaji atafakari zaidi kuhusu jambo linalozunguziwa ndiposa afahamu kwa kina. Mtunzi anaweza kutumia maswali ya balagha wakati anataka kuwatia hadhira moyo.

Mfano wa swali balagha unapatikana katika *Utenzi wa Al-Inkishafi* ubeti wa 11;

**Moyo wangu nini huzundukani!**
**Likughurielo, hela ni n'ni?**

Swali la Balagha linajidhihirisha katika mshororo wa pili wa ubeti huu.

#### 2.6.3.6 Nidaa

Katika matumizi ya mbinu ya nidaa, mtunzi hutumia alama za hisi katika kazi yake kuonyesha mshangao au msisitizo wa jambo lililosemwa. Nidaa pia hutumika kubebea

hisia mbalimbali za wahusika katika kazi za kifasihi kama vile: uchungu, furaha, masikitiko na mshangao.

Mfano wa mbinu ya nidaa unapatikana katika *Utenzi Al-Inkishafi* ubeti wa 11;

**Moyo wangu nini huzundukani!**

Likughurielo, hela ni n'ni?

Nidaa inajitokeza katika mshororo wa kwanza wa ubeti unaonukuliwa hapo juu kuonyesha mshangao.

### 2.6.3.7 Methali

Methali ni usemi wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Methali hutumika kwa lengo la kuonya, kuelimisha, kuhimiza au hata kumbeza mtu au jamii. Methali hutumiwa kwa wingi hasa katika kazi za fasihi za kinathari. Katika kazi za kishairi na hasa tendi, methali huwa hazitumiwi sana.

### 2.6.3.8 Takriri

Takriri ni mbinu ambayo hutumika na mtunzi kurejelea urudiaji wa sauti fulani, herufi, maneno au mstari fulani katika kazi za kifasihi. Nia ya mtunzi anapotumia mbinu hiyo huwa ni kuleta msisitizo katika ushairi wa kimapokeo wa Kiswahili. Takriri inayojitokeza sana ni ile ya vina, ambapo sauti fulani inarudiwa katika mishororo ya shairi. Takriri pia inaweza kuwa ya sauti au ikawa ya maneno.

#### 2.6.3.9 Visawe

Visawe ni maneno yanayoendelezwa au kutamkwa tofauti lakini yanabeba maana sawa. Msanii hutumia visawe kwa kuonyesha ujuzi alio nao katika kubadilisha msamiati wake ili kuonyesha maana hiyo hiyo iliyokusudiwa. Pia hutumia visawe kwa kutaka kumtia motisha msomaji wake aendelee kusoma. Jambo hili ni kwa sababu maneno yakirudiwarudiwa huchosha. Kisawe kinaweza kuwa cha mahali, mhusika, kifaa au wazo fulani.

#### 2.6.3.10 Misemo

Misemo ni matumizi ya maneno ya kawaida kijozi kwa njia isiyokuwa ya kawaida. Misemo huhitaji mtu kufikiria kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Misemo mingi hubuniwa na jamii. Misemo katika jamii moja hutofautiana na jamii nyingine. Hii ni kwa sababu baadhi ya misemo hutungwa kutokana na mazingira pamoja na itikadi za jamii. Misemo hutumika kwa lengo la kusitiri maana na pia kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo. Mifano ya misemo katika Kiswahili ni:

**Kata kamba** (aga dunia), **lia ngoa** (ona wivu), **fanya hima** (fanya haraka), **fanya vitimbi** (zusha mambo, leta fujo), **palia makaa** (jiletea taabu).

#### 2.6.3.11 Tanakali za sauti

'Tanakali' ni neno ambalo linaiga sauti fulani, jinsi kitu kiangukavyo au kiliavyo. Mshairi hutumia tanakali kwa nia ya kumwezesha msomaji kupata taswira kamili na hisia za mlio wa kitu kinachozungumziwa.

Katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani* ubeti wa 20 tunapata usemi ufuatao, "…tatu ndio ke-ke-ke"

### 2.6.3.12 Taashira / Ishara

Taashira ni aina ya tamathali ya usemi ambapo jina la kitu hutumiwa kuwakilisha kitu kamili au kitu au tukio fulani linaloficha maana mahsusi katika kazi ya kifasihi. Lazima kuwepo na uhusiano baina ya vitu fulani vinavyohusishwa ndio viweze kuibua fikra fulani katika akili ya msomaji. Kuhusu hoja hii, Kuhenga (k.h.j:18) anasema kwamba, "kwa sababu ya mwambatano wa ujamii au uhusiano mkubwa uliopo kati ya vitu fulani, ishara, alama, dalili au neno fulani hutumiwa kuwasilisha tendo au kitu tupendacho kutaja badala ya kuelezea waziwazi". Hivyo, taashira hutumika kuwasilisha kitu ambacho mtu hangependa kukitaja moja kwa moja. Kwa mfano, mtu anaweza kusema ya kwamba "safari yetu ilikuwa ya vigelegele". Katika mfano huu, neno 'vigelegele' linaashiria furaha. Pia linaweza kuamaanisha kuwa safari ilikuwa ya kupendeza au bila matatizo yoyote.

## 2.7 HITIMISHO.

Sura hii imehusu uelezeaji wa misingi ya kuhakiki fani. Tumejadili dhana ya fani na kuonyesha vipengele vyake muhimu. Pia, tumejadili vipengele vya fani ambavyo tutavishughulikia katika sura ya tatu, nne na tano. Vipengele vyenyewe ni pamoja na msuko, muundo, mandhari, wahusika na matumizi ya lugha. Katika sura ya tatu, tunahakiki msuko na muundo katika *Utenzi wa Tambuka.*

# SURA YA TATU

# MSUKO NA MUUNDO KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*.

## 3.0 UTANGULIZI

Sura hii inahusu msuko na muundo wa *Utenzi wa Tambuka*. Tumeamua kuvishughulikia vipengele hivi pamoja katika sura hii kwa sababu vina uhusiano wa karibu mno. Tutaanza na kipengele cha msuko na hatimaye cha muundo. Tutatoa mifano ya hapa na pale kutoka kwa utenzi wenyewe.

## 3.1 MSUKO KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

Katika sura ya pili, tulieleza msuko kuwa mfuatano wa matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi. Mfuatano huu hutegemea uhusiano wa kiusababishi.

Msuko wa *Utenzi wa Tambuka* ni changamano au msuko wa msago. Vilevile, msuko huu umechanganya msuko mkuu na msuko kinzani.

Matendo katika utenzi huu yamepangwa katika ule uhusiano wa kiusababishi. Japo si wazi, vinaeleweka. Msanii ameanza utenzi kwa mtindo uliozoeleka katika tenzi nyingi wa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kuanzia ubeti 1-12, anamsifu Mungu na Mtume Muhammadi. Kisha, katika ubeti wa 12 mtunzi anaitisha kalamu nzuri ya kuandika akisema kuwa anataka kusimulia kisa au hadithi ya Kiarabu. Msanii ameanza masimulizi kwa habari za tanzia ambapo Jaafari, mpwaye Muhammadi pamoja na Waislamu wengine wameuawa wakiwa katika mikono ya Wakristo wa Tambuka. Haya

yanasimuliwa katika beti za 14-17. Muhammadi anaanza kuomboleza kwa siku saba. Hatimaye Muhammadi anawaambia watu wote wajiandae kwa vita. Hatua hii inachukuliwa baada ya kupata ujumbe kutoka kwa malaika Jibrili kuwa Mungu anamtaka Muhammadi kwenda Tambuka kulipiza kisasi kufuatia kifo cha Jaafari na Waislamu wengine. Haya yanasimuliwa katika beti za 22-28.

Katika harakati za maandalizi kwa vita, mtunzi anasimulia kuhusu safari ya Hattari kwenda Tambuka kumpelekea mfalme Herekali barua. Tunaelezwa jinsi Hattari anamwandaa farasi wake hata anatunga shairi kumhusu Mtume Muhammadi kule jangwani. Safari yenyewe inachukua siku kumi. Haya yanasimuliwa katika beti 82-107.

Kisha, mtunzi anasimulia kuhusu majibu ya Askofu kupitia kwa barua akidai kuwa yuko tayari kwa vita. Majibu hayo yanamkasirisha kila mhusika Mwislamu. Mtume Muhammadi anakusanya makabila ya Kiarabu kuungana ili kupigana dhidi ya Wakristo. Majeshi mbalimbali ya Waarabu yanaanza kuwasili moja baada ya jingine kwa mtindo tofautitofauti ili kujiandaa kwa vita. Haya yanasimuliwa katika beti za 204-253.

Baada ya makabila yote kuingia, Mtume Muhammadi analiamuru jeshi lake kukusanya chakula na vitu vingine muhimu kwa safari yao. Hakuna mmoja aliye na chakula cha kutosha isipokuwa Athumani. Athumani anakataa kuwauzia majeshi hayo chakula kwa vyovyote vile. Muhammadi anapohusika, Athumani anaamua kuwapa bila malipo ila apewe ahadi ya kuingia peponi. Baada ya kuahidiwa Peponi, Athumani anakubali kuwapa majeshi ya Muhammadi chakula. Hata hivyo, chakula hicho hakitoshi. Hapo

ndipo Mtume Muhammadi anayaongoza majeshi yake kwenye uwanja wa zitango / matango ambayo hayapendwi na watu na kisha kuwaambia wayatunde na kuyaweka makwao. Haya yanasimuliwa katika beti za 294-296. Mtunzi anasimulia kuwa kila mmoja anayatunda matango bila ya kulalamika isipokuwa Mughera, ambaye ana shaka moyoni mwake kuhusu maagizo ya Muhammadi.

Baada ya Mughera kuyatunda matango, anayatupa na kusalia na matatu tu. Abu Salama anamwona Mughera akifanya hivyo na anamwarifu Muhammadi. Kutokana na hamu ya kutaka kujua ikiwa matango hayo ni tofauti na yale anayoyajua, Mughera anachukua moja na kuvunja. Ajabu ni kwamba anaona kuwa mle ndani mna asali na samli. Jambo hili linamfanya ajute na kutubu. Mughera anajitenga na kwenda mahali pweke na kuanza kufikiria jinsi atakavyojitia kitanzi. Katika hali hiyo, Mungu anamwona na kumtuma malaika Jibrili kumwambia Muhammadi amsamehe.

Baada ya kisa hiki, jeshi linaachiliwa kurudi nyumbani kwenda kujiandaa kwa ajili ya vita vitakatifu. Vita hivi vinanuiwa kuwapa wapiganaji wa Kiislamu nafasi ya kuingia Paradiso.

Jeshi linapokaribia kuanza vita, Malaika Jibrili anakuja na ujumbe kuwa Ali bin Talib, shujaa wa mashujaa hatashiriki katika vita kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameamuru kuwa Ali abaki Madina. Majeshi ya Muhammadi yanakuwa na shaka moyoni mwao lakini hawana uwezo wa kumpinga Mungu. Jeshi linaanza safari. Linapofika katika bonde la jangwa la Hijabu, wanapata mtu mmoja anayeishi humo akijulikana kama Karari. Karari ameelezwa kuwa msomi wa hali ya juu na pia ni Mwislamu. Karari

hajawahi kukutana na Mtume Muhammadi lakini ameshika sana imani ya Muhammadi. Kwa ukarimu wake, Karari anamwalika Mtume Muhammadi pamoja na jeshi la watu sabini na saba elfu kuwa naye kwake. Anawapa chakula katika vyano vyao. Kila chano kinatumiwa na watu kumi. Kila mmoja anakula chakula na kushiba hata kunakuwa na masazo. Kisha anawapa majamvi kulalia. Keshoye, Karari anamuaga Muhammadi pamoja na jeshi lake na anapata fursa ya kuthibitisha kuwa Muhammadi ndiye Mtume aliyewahi kumsoma katika vitabu vitakatifu na kuwa yeye ndiye mtume wa mwisho. Kupitia kwa muujiza wa chakula ambapo watu elfu na saba wanakula na kubakisha chakula, pia ulimthibitishia kuwa Mtume aliyetabiriwa ameshakuja.

Hatimaye, jeshi linafika jijini Tambuka anapoishi Herekali. Miungu ya Wakristo ndiyo inayowavutia sana ingawaje kwao ni kufuru. Herekali anapoona kuwa jeshi la Muhammadi limewasili Tambuka, naye anatuma lake lenye takribani majeshi 80,000. Jeshi hili linaongozwa na Sayari. Kwa bahati mbaya, Sayari anauawa katika vita vya awamu ya kwanza. Wakristo wanafurahia ushindi huo na kunyakua mali ya Waislamu kambini. Warumu wanaendelea kuongezeka lakini baadaye wanashindwa na Waislamu. Mwishowe, wanaenda kujiangusha miguuni pa Waislamu na wanakiri imani ya dini hiyo na hatimaye wanasilimu. Hatua hii ni ishara ya kusalimu amri.

Mtunzi anasimulia kuwa vita baina ya Waarabu na Warumu vilifanyika katika awamu sita. Kila wakati Waarabu wanashindwa isipokuwa katika vita vyao vya sita ambapo wanapokuwa wanakaribia kushindwa, Mungu anaingilia kati. Mungu anamtuma Malaika Jibrili kumtia Mtume Muhammadi nguvu na pia kumweleza kuwa Mungu yuko

pamoja nao, wasife moyo. Kufikia hapa, Mtume Muhammadi anaamuriwa na Mungu amwite Ali aje kushiriki katika vita. Wakati huu Shehe Ali yuko nyumbani akimshughulika mkewe. Anaposikia sauti ya Mtume Muhammadi ambaye pia ni baba mkwe wake, anaitikia mwito huo.

Anapofika Madina, Ali anapewa mawaidha na maagizo na Mtume Muhammadi kuhusu vita hivyo. Anasema kuwa lazima ashinde Herekali ndipo vizazi vijavyo viwe na kumbukumbu ya ushindi wa Uislamu. Ali anapokea upanga uitwao Dhuli Fikari. Anapoonekana vitani, watu wanafikiri kwamba ni Mtume Muhammadi aliyeungana nao vitani. Ni mtumwa mmoja tu ambaye anamtambua Ali. Ubishi unazuka hatimaye, kwani kiongozi wao naye anadai kuwa Ali yuko Madina. Ubishi huo unaenea sana kwani mtumwa huyo anaahidiwa zawadi iwapo itatokea kuwa Ali yuko nao vitani. Kwa lengo la kukomesha ubishi huo, mtumwa huyo anaamua kuingia katikati ya vita na kumwona Ali akiwa anapambana na maadui wake. Ali anataka kuthibitisha kuwa yeye ndiye kwa kumkaribia na hata kumuuliza jina. Ali anamwambia kuwa yeye ni babake Hassani.

Vita kama vinavyosimuliwa katika utenzi huu ni vikali mno. Warumu wanapopigwa katika vita hivyo, wanakimbilia usalama upande wa Herekali lakini Herekali anatafuta palipo na usalama. Baada ya muda mchache, jeshi la Warumu linatoroka wakiwa na hofu mioyoni mwao. Kwa upande mwingine, Shekhe Ali Diriama (Simba) anawafuata nyuma kwa karibu. Anataka kuwateka nyara na kukusanya miungu yao bila ya kutoa sauti wala kumpiga vita. Hali hii inaonyesha kuwa Warumu wamepoteza matumaini. Kwa vyovyote vile, hawaoni wakikaribia ushindi.

Vita vya Tambuka vinaishia hapo. Waisilamu wanaibuka washindi. Herekali na Askofu wake wanakamatwa na kufungwa minyororo na kuletwa mbele ya Mtume Muhammadi. Hatimaye, Mtume Muhammadi anamwombea Ali dua ya kufika Madina salama. Ali anang'oa nanga kwenda nyumbani na anapokelewa vyema na mkewe.

Kufikia hapa, tunaona kuwa msuko wa *Utenzi wa Tambuka* ni msuko msago au changamano kwani unaenda nyuma na mbele kila mara. Vilevile, msuko huu umehusisha msuko mkuu ambapo ni kisa kikuu kinachomhusu Mtume Muhammadi anavyopambana na maadui wake ambao ni Wakristo. Pia kuna msuko kinzani ambao unahusu jitihada za mhusika mkuu mpinzani ambaye ni Herekali na vile anavyokabiliana na mashambulizi ya Mtume Muhammadi

Ingawa *Utenzi wa Tambuka* ni mrefu sana, mtunzi ameweza kuupa msuko wake mshikamano. Visa vimefuatana vizuri kiusababishi. Pia kuna taharuki zinazowapa wasomaji hamu ya kufuatilia masimulizi yenyewe kwa makini. Msuko huu pia umeingiliana na kipengele cha kimaandhari na cha wahusika kwani ni kutokana na msuko huu ndipo tunaona mandhari mbalimbali na matendo ya wahusika katika mandhari hayo.

### 3.2.0 MUUNDO KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

Katika sura ya pili tuliona kuwa kuna muundo wa ki-vitushi, muundo wa ndani na muundo wan nje. Tunaona kuwa muundo wa ki-vitushi na muundo wa nje unaingiliana

na msuko. Kwa hivyo, katika utafiti huu, tunaujadili muundo wa nje wa *Utenzi wa Tambuka*.

### 3.2.1 Muundo wa nje

Muundo wa nje wa tenzi unahusu urefu, beti, mishororo, vipande, mizani, vina na kibwagizo.

*Utenzi wa Tambuka* una jumla ya beti elfu moja mia moja na hamsini. Idadi hii kubwa ya beti inaufanya utenzi huu kuwa miongoni mwa tenzi ndefu sana za Kiswahili. Kila ubeti wa *Utenzi wa Tambuka* umegawanywa katika mishororo minne kama yalivyo mashairi ya tarbia. Pia, kuwa na mishororo minne katika kila ubeti ni mojawapo wa kaida za tenzi. Ufuatao ni ubeti wa tatu wa *Utenzi wa Tambuka* kuonyesha mishororo:

Ubeti wa 3; Kumuhimidi Jabbari
ndilo jawabu hiari
na kusallia Basiri
ni jawabu afudaa.

Kila mshororo wa *Utenzi wa Tambuka* ni kipande kimoja tu. Yaani, mishororo haijagawanywa katika vipande zaidi. Ni kaida ya tenzi kuwa mshororo uwe ni kipande kimoja tu.

Kila mshororo wa kila ubeti una mizani minane. Ni kaida ya tenzi kuwa na mizani chini ya kumi na mbili. Baadhi ya tenzi huwa na mizani kumi na miwili na nyingine huwa na

mizani sita kwa kila ubeti. Hata hivyo tenzi nyingi huwa na mizani minane katika kila ubeti kama ilivyo na *Utenzi wa Tambuka*. Tutatoa mfano kutoka ubeti wa 12:

Kha-za-i-ni-to hi-bu-ri
1- 2- 3-4- 5 6- 7- 8

Na ka-la-mu a-hi-a-ri
1 2- 3- 4 5-6- 7-8

Kha-pi-ja-to mi-si-ta-ri
1- 2-3 -4 5- 6- 7-8

Ya Wa-ru-mu na Ra-su-a
1 2- 3- 4 5 6- 7- 8

Vina vya mishororo ya *Utenzi wa Tambuka* vinabadilikabadilika kutoka ubeti hadi mwingine isipokuwa kina '**a**' cha mshororo wa mwisho ambacho kinakaririwa katika utenzi wote kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kina hiki hujulikana kama bahari. Tunatoa mfano katika beti za 25 na 26:

Ubeti wa 25

Ondoka wewe habi**bu**

Pamoja na asiha**bu**

Wamakka na Yathiri**bu**

andamani nyuthe ndi**a**

Ubeti wa 26

Ondokani nyuthe mwe**nde**

Tambuka mukaipa**nde**

na lipesho mute**nde**

mulipe kyenu kiko**a**

*Utenzi wa Tambuka* hauna kibwagizo. Mshororo wa mwisho umebadilikabadilika kutoka ubeti hadi mwingine.

Kwa ujumla, mtunzi amefanikiwa kutekeleza kaida za kimuundo za utunzi wa tenzi. Ijapokuwa utenzi wenyewe ni mrefu, mtuzi ameweza kutosheleza sheria au kaida hizo bila kukosea. Hivyo, ameonyesha ufundi wa hali ya juu kabisa.

## 3.3 HITIMISHO

Sura hii imehusu uhakiki wa msuko na muundo wa *Utenzi wa Tambuka*. Tumeona kuwa msuko ni wa msago au changamano. Pia, tumeona kuwa muundo wa nje umefuata kaida za utunzi wa tenzi. Mtunzi ameonyesha utaalamu na ujuzi wake mkubwa katika utunzi.

# SURA YA NNE

# MANDHARI NA WAHUSIKA KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tunahakiki ujenzi wa mandhari na uumbaji wa wahusika katika utenzi huu. Tunadhamiria kuonyesha dhima ya mandhari na wahusika katika utenzi huu. Pia, tunatathmini kufana au kutofana kwa mtuzi katika ujenzi wa mandhari na uumbaji wa wahusika.

## 4.1.0 MANDHARI KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

Mazingira ya usimulizi ni wazi kabisa katika utenzi huu. Utenzi unapoanza, msanii anarejelea mandhari ya nyumbani ambapo Mtume Muhammadi anapokea ujumbe wa tanzia akiwa na jamaa zake. Wanaomboleza kwa siku saba kama ilivyo desturi katika dini ya Kiislamu. Haya yanasimuliwa katika beti za 14-24.

Mazingira ya kinyumbani yanajitokeza ambapo Shehe Ali anapata ujumbe akiwa Madina akimsaidia mkewe kazi. Ali anaitikia mwito huo na kukimbia moja kwa moja kwenye vita huko Tambuka. Baada ya vita, Mtume Muhammadi anamuombea Ali dua ya mwisho kisha anarudi nyumbani. Mtunzi amerejelea mandhari ya kinyumbani kwa kutuonyesha jinsi mkewe Ali anavyomlaki kwa heshima na unyenyekevu. Isitoshe, anamsaili kwa kutaka kujua zaidi kuhusu vita. Haya yanaonekana katika beti za 1091-1101.

Mfano:

Ubeti wa 1094;

**Mwenye kungia nyumbani,**

***Shekhe Aba li Hasani,***

**Mwana binti Amini,**

**nyaoni kamwangukia.**

Mandhari haya yametumiwa na mtunzi kuwasilisha maudhui ya nafasi ya mwanamke. Mkewe Ali anatumiwa kama mfano bora kwa wanawake wengine na kuwapa funzo la namna ya kuwashughulikia waume wao wanapotoka katika shughuli nzito kama hiyo. Pia, anatumiwa kuonyesha mchango wa kisaikolojia wa wanawake katika vita vya Tambuka. Isitoshe, mandhari haya ya nyumbani yanaonyesha maudhui ya mapenzi na uhusiano mwema kati ya Ali, mkewe na mwanawe Hassani.

Katika utenzi huu, maeneo ya Kijiografia yanatajwa. Kwa mfano, Madina ni mahali anakoishi Mtume Muhammadi na pia Ali. Baada ya vita vya ufanisi, Ali anarudi nyumbani kwake Madina. Mtunzi vilevile amerejelea mji wa Tambuka alikokwenda mfalme Herekali kwa ajili ya vita. Hapo ndipo Waislamu wanaenda na kuanzisha vita kwa nia ya kulipiza kisasi kufuatia kifo cha Jaafari mpwawe Mtume Muhammadi. Nchi ya Rumu imerejelewa kwani Hattari anapopewa barua na Mtume Muhammadi anapeleka kule Rumu. Maeneo haya ya Kijiografia ni maeneo halisi yanayopatikana katika ulimwengu halisi kule Uarabuni. Maeneo haya ya kijiografia ndimo vita vya kihistoria vilimotukia. Sababu za kutumia maeneo haya ni kuupa *Utenzi wa Tambuka*

uhalisia fulani kwani licha ya kuwa utenzi huu ni kazi ya kisanaa, pia una majukumu ya kidini. Matumizi ya mandhari haya pia yanaonyesha kuwa mtunzi huyu ana uwezo wa kuyafinyanga matukio halisi kisanaa.

Mandhari ya jangwani pia yamerejelewa. Tunaona haya katika safari ya Hattari anayesafiri jangwani kwa farasi wake kutoka Madina kuelekea mjini Tambuka. Ali anachukua takribani siku kumi kufika nchi ya Rumu ili kuwasilisha ujumbe wa vita. Haya yanasimuliwa katika beti za 95-106. Mazingira ya jangwani yanaonekana pia katika vita vya awamu ya sita. Hapa ndipo vita vinakuwa vikali sana. Inabidi Mungu ajidhihirishe. Mungu anamtuma Malaika Jibrili kwa Mtume Muhammadi kumwambia ya kwamba aondoe sikitiko moyoni. Haya yanatokea baada ya Mtume Muhammadi kupaaza sauti inayosikika katika jangwa lote.

Ali anapoitwa na Mtume Muhammadi kuja kujiunga na jeshi, anamwandaa farasi wake kutoka Madina na kufunga safari kupitia jangwani. Anapanda milimani na kuteremka mabondeni kuelekea Tambuka kwenye uwanja wa vita. Mandhari haya ya jangwani yametumiwa kuonyesha shida na matatizo wanayopitia Waislamu katika vita hivi. Tunaona kwa mfano jua ni kali mno, hawana chakula cha kutosha na wanakosa maji. Hata hivyo, Waislamu wanavumilia hadi wanashinda. Hivyo, mandhari haya ya jangwani yanasawiri maudhui ya uvumilivu na imani. Pia, mandhari haya yanachangia kuonyesha maudhui ya miujiza kwa sababu Mtume Muhammadi anatekeleza miujiza ya chakula.

Mtunzi amefaulu katika kutuchorea mazingira ya utawala na vyeo. Bwana Hattari anapopeleka barua Tambuka, anampa Askofu ambaye anampelekea mfalme Herekali. Kupitia kwa hatua zote hizi tunaona kuwa ni mfalme Herekali tu aliye na uwezo wa kuishughulikia barua ile. Iwapo mwingine angeishughulikia, basi uamuzi wa Herekali ulitegemewa sana. Tunamwona mfalme Herekali katika mazingira ya kiutawala na uwezo mkuu. Yeye ndiye anayesimama kidete na kumwambia Hattari kuhusu nia yake ya kumshambulia Mtume Muhammadi na jeshi lake. Hata hivyo, mtunzi hajatuchorea mandhari ya ikulu yenyewe. Hatupati sura yake kamili.

Kunayo mandhari ya kidini. Muhammadi na jeshi lake wanawakilisha mandhari ya dini ya Kiislamu huku Herekali na jeshi lake wakiwakilisha dini ya Kikristo. Vilevile, kuna mandhari ya makafiri na yale ya waumini ambao wanapatikana Madina.

Mandhari ya dini ya Kiislamu yanajitokeza kwa sala mara kwa mara. Vita vinapokuwa vikali sana Mtume Muhammadi anasali kisha Mungu anatuma Malaika wake kuleta ujumbe wa kufana. Dini ya Kikristo inapewa mazingira ambapo wanaonekana wakiwa wamebeba sanamu. Jukumu la mandhari haya ni kuwasawiri Waislamu kuwa wacha Mungu na wenye mienendo myema huku Wakristo wakiwasilishwa kama wasio na dini au waabuduo shetani kupitia kwa sanamu.

Pia katika *Utenzi wa Tambuka* tunapata mandhari ya kidhahania ambapo wahusika kama vile Mungu na Malaika Jibrili wanaishi mbinguni. Waumini wanapotoa sala zao, Mungu anajibu na kutuma Malaika Jibrili. Mtume Muhammadi ndiye anayeunganisha watu na

Mungu pamoja na ulimwengu wa kiroho. Anaombea jeshi lake katika hali yao ya sintofahamu (Tazama ubeti wa 37). Kando na haya yote, msanii hajatupa sura yoyote ya mbinguni. Kwetu sisi, mbinguni kumebaki kuwa dhahania tu akilini mwetu.

Mtunzi ameonyesha mandhari ya kivita katika utenzi huu. Baada ya kuomboleza kwa siku saba, Mtume Muhammadi anawaambia Waarabu wote kuwa ni sharti waende Tambuka kulipiza kisasi na kutenda liwapasalo. Kwa ghafla, Muhammadi anamwamuru Shehe Ali kuandika barua ya vita ili imuendee mfalme Herakali. Baada ya kupata majibu kutoka Tambuka, Muhammadi anaamuru Shehe Ali kuandika barua nyingine kwa makabila yote ya Waarabu. Lengo kuu likiwa kuwaalika waje kushambulia Warumu kwenye mji wa Tambuka. Katika ubeti wa 26, Mungu anamwambia Muhammadi:

**Ondokani nyuthe mwende,**

**Tambuka mukaipande,**

**na lipeselo mutende'**

**mulipe kyenu kikoa**.

Tunaona pia mandhari ya kivita pale Tambuka. Jeshi la Kiislamu linawasili tayari kushambulia. Warumu nao wanajitokeza wakiwa tayari na sanamu zao huku wakipiga ngoma na tarumbeta. Waumini wa dini ya Kiislamu wanapaaza sauti na kusema ya kuwa "hakuna Mungu ila Allah". Haya yanaonekana katika beti za 460, 467-474. Katika mandhari haya ya kivita, kunayo pia mandhari ya sala. Waislamu wanamuomba Mungu

kabla ya kukabiliana na Warumu katika vita. Maombi haya yanaleta ufanisi kwani nyakati hizi zote wanaibuka washindi. Mandari haya ya kivita na sala yanatumiwa kuonyesha maudhui ya vita na athari zake. Pia yanaonyesha maudhui ya ushujaa na ujasiri ambapo tunaona kuwa wahusika wa pande zote wanapigana kwa ujasiri bila kuogopa. Funzo linalotokana na mandhari haya hasa kwa Waislamu ni kuwa maombi yanasaidia na wanafaa kumwomba Mungu katika hali yoyote ile na Mungu atawaokoa.

Vilevile, mshairi ametufafanulia mandhari ya kimiujiza. Mtume Muhammadi anapoandaa jeshi lake kwa ajili ya vita, anajali maslahi yao ya chakula. Katika beti za 296-310, tunaona Muhammadi akiwaongoza jeshi lake kwenye shamba la matango. Matango ni matunda ambayo hayavutii sana watu wengi; hayana ladha kamwe. Muhammadi analiamuru jeshi lake kuyatunda matango. Wote wanayatunda bila tashwishi isipokuwa Mughera ambaye ana tashwishi moyoni. Baada ya kupasua yale matango, Mughera anagundua kuwa yana asali na samli. Mughera anafurahi sana anapogundua huo muujiza. Ajabu ni kwamba tayari Mughera ameyatupa yale matango anapogundua uzuri wake.

Muujiza mwingine unabainika katika jangwa la Hijabu. Hapa ni mahali ambapo panaishi mtu mmoja pekee kwa jina la Karari. Karari ni muumini wa Kiislamu lakini hajawahi kukutana na Mtume Muhammadi. Anapomwona Muhammadi, Karari anamkaribisha pamoja na jeshi lake kwa chajio. Jeshi lenyewe ni la watu takribani 77,000. Karari anawapa chakula kwenye vyano. Baada ya Muhammadi kumwomba Mwenyezi Mungu, watu wanakula chakula hicho, wanatosheka na hata kinasalia. Karari anapoona hayo,

ananyenyekea na kuinama chini kisha kuabudu Mwenyezi Mungu. Haya yanadhihirika katika beti za 420-422. Mandhari haya ya kimuujiza yanajenga maudhui ya miujiza dini na imani. Yanatumika kujenga wasifu wa wahusika wa Kiislamu kama wanaomcha Mungu na kuwa na imani ya hali ya juu.

Kwa ujumla, msanii amefana katika ujenzi wa mandhari ya *Utenzi wa Tambuka*. Mandhari ya jangwani ni bora zaidi kwa vita. Aina hii ya mandhari hupatikana kule Uarabuni, ambako kuna maeneo yenye majangwa. Msanii ametumia baadhi ya wahusika kama Ali na Hattari ambao wanasafiri jangwani pekee yao usiku na mchana bila kushambuliwa na hayawani. Hali hii ni ithibati bayana kuwa Mungu anawawezesha Waarabu kushinda vita na daima yuko nao jangwani.

Wahusika kama vile Mungu na Malaika wametengewa mandhari ya kidhahania yanayofaa, yaani mbinguni. Hatutarajii Mungu na Malaika wake kuishi popote pale ila mbinguni. Hali hii inafanya usimulizi huu kuwa na misingi ya kidini. Sehemu hii imedhihirisha mwingiliano uliopo baina ya mandhari, uumbaji wa wahusika na maudhui ya *Utenzi wa Tambuka*.

### 4.2.0 WAHUSIKA KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

Katika utenzi huu, mtunzi amewasawiri wahusika mbalimbali, wao ni pamoja na Mtume Muhammadi, Ali, Mungu, Jibrili, Herekali, Askofu Waziri, Mkewe Ali, Jasusi, Sayari, Rahibu, Karari na Mughera. Wahusika hawa wote wamesawiriwa na mtunzi kwa namna

ambavyo sifa zao zadhihirika wazi. Upo ukinzani unaojionyesha wazi katika wahusika hawa. Kuna kikundi cha Waislamu kinachokinzana na kikundi cha Wakristo. Kikundi cha Wakristo kina shujaa wake Herekali. Waislamu wanaye shujaa wao kwa jina Ali.

Tutaangalia baadhi ya wahusika katika *Utenzi wa Tambuka* kwa kuangalia sifa zao na kuthibitisha kuwepo kwao katika utenzi. Ili kuweza kushughulikia uchanganuzi huu kwa njia iliyo wazi, tumewagawa wahusika katika makundi matatu makuu: wahusika wa Kiislamu, wahusika wa Kikristo na Wahusika wanaobadilika.

#### 4.2.1.0 Wahusika wa Kiislamu

Wahusika tunaowaita wa Kiislamu ni wale ambao wanafuata dini ya Kiislamu, wanamtambua Mtume Muhammadi kuwa kiongozi wao na pia wanachangia kwa njia moja au nyingine katika kuendeleza dini ya Kiislamu katika *Utenzi wa Tambuka*.

#### 4.2.1.1 Mtume Muhammadi

Mtume Muhammadi ni mhusika mkuu katika *Utenzi wa Tambuka*. Anaenda vitani lakini hashiriki katika vita kwa njia ya moja kwa moja. Jukumu lake kuu ni kuliunganisha jeshi lake na Allah. Muhammadi ni amiri jeshi mkuu wa jeshi la Kiislamu. Ujumbe unapokuja kutoka kwa Mungu, unapitia kwake. Ni yeye anayewatia moyo Waiislamu vita vinapokuwa vikali. Mtume Muhammadi vilevile anachukua jukumu la kuwasifu majeshi yake na kuwakumbusha ahadi za Paradiso, ambazo zinawapa nguvu ya kupigana zaidi.

Mtume Muhammadi ana usufii wa moyo. Ni yeye amwonaye Jibrili anapotokea na aliwahi kwenda mpaka mbingu la saba alikoonana na Allah uso kwa uso na kupewa amri za kuishi duniani.

Muhammadi amechorwa kama kiongozi mwenye uwezo wa kuwaleta Waarabu pamoja kumshambulia Herekali. Tunaona namna Waarabu wanavyochangamkia vita wakati Muhammadi anapowaandikia barua akiwataka wajiandae kwa vita.

Muhammadi anasemekana kuwa aliyeumbwa vizuri zaidi kuliko mwanadamu mwingine yeyote. Tunaona kuwa jasusi wa Herekali anapoingia kambini kujua idadi ya majeshi ya Muhammadi, anapoletwa mbele ya Mtume Muhammadi, anashangazwa na utukufu alio nao. Uso wake unang'ara na ana uzuri usioweza kulinganishwa na mwingine. Sifa nyingine ya msamaha inaonekana katika hali hii kwani tunamwona Mtume Muhammadi akimsamehe Jasusi huyu na hata kumwachilia na kumruhusu arudi Rumu.

Mtume Muhammadi ni mtiifu. Anatii amri ya Mungu ya kumtaka aanzisha vita hivi kwa sababu ya kulipia kifo cha Jaafari-mpwaye Mtume Muhammadi.

Kwa ujumla, Muhammadi amesawiriwa kama mshirika mkuu wa Mwenyezi Mungu, ambaye anatumiwa na Mungu kupigana dhidi ya ukatitili wa Herekali na Wakristo.

#### 4.2.1.2 Ali

Sawa na Muhammadi, Ali ni mhusika mkuu katika *Utenzi wa Tambuka*. Ni mkwewe Mtume Muhammadi. Ali ni mtiifu. Tunaona kuwa anapopata amri kutoka kwa Allah kuwa asiende vitani anatii.

Vilevile, Ali ameajibika kama mume. Tunamwona akimsaidia mkewe kazi pale nyumbani mpaka sauti ya Mtume Muhammadi inapomwita. Mtunzi amamtumia kama kielelezo cha wanaume ambao wanapenda familia zao na wako tayari kuwatumikia kwa kila hali.

Ali amechorwa kama mhusika shujaa wa Waislamu. Hata anapewa jina Haidari, yaani Simba. Wanapoaanza safari ya kwenda Tambuka anaamrishwa na Allah abaki Madina. Wenzake wanashangaa iwapo watashinda vita bila yeye. Hata hivyo, wanajipa moyo kuendelea kwa sababu amri ilitoka kwa Allah na hakuna yeyote anayeweza kumpinga. Ushujaa wake unaonekana bayana anapoitwa dakika ya mwisho kuwaokoa Waislamu. Anafaulu kwa kiasi kikubwa kuwaua wengi na hata kuchukua mali yao anayoileta kwa Mtume Muhammadi. Jukumu lake katika hali hii ni kuwasilisha maudhui ya ushujaa.

Ali ni mtu wa kujinaki. Anasema kuwa yeye ni Simba na Ndovu wa Allah. Yeye ndiye wa kuwatia machungu makufari na kuwa ana tajriba ya kuwanasa. Anajidai kuwa dhuli fikari aliyompa Mola ni upanga mwema ulioandikiwa yeye kuutumia.

Kwa ujumla, Ali amechorwa kama mhusika jasiri na mshirika mkuu wa Mtume Muhammadi katika kupigana dhidi ya ukafiri.

#### 4.2.1.3 Mwenyezi Mungu

Mungu ni mhusika asiyeonekana lakini anaaminiwa kuwa anaishi mbinguni. Ni mhusika msaidizi na shujaa wa Kiislamu kwani tunaona akimsaidia Mtume Muhammadi katika vita baina yake na Wakristo. Kila mara, Mungu anawasiliana na Mtume Muhammadi kupitia kwa Malaika wake mkuu Jibrili na kumpa mwelekeo na mawaidha vitani.

Mungu ameelezwa kuwa muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo. Ameelezwa kuwa asiye na mke wala mwana. Hana mfano na hivyo hastahili kulinganishwa na kitu au mtu yeyote.

Pia Mungu ameelezwa kuwa ndiye atakayekuwa hakimu siku ya Kiyama. Atawalipa wanadamu wote kulingana na matendo yao. Yeye tu ndiye anayestahili kuabudiwa.

Mungu hapendi maovu wala kiburi chochote. Ni kutokana na ukatili na kiburi cha Mfalme Herekali dhidi ya Wakristo ndipo Mwenyezi Mungu anamwamuru Mtume Muhammadi kuchukua hatua ya kulipiza kisasi. Hatua hii ni ishara ya mapenzi ya Mungu kwa Waislamu.

Majukumu ya Mwenyezi Mungu katika *Utenzi wa Tambuka* ni kuwasilisha maudhui ya kidini na ushujaa. Pamoja na kwamba ndiye wa pekee wa kuabudiwa, Mungu anaonyesha mwegemeo wake kwa dini ya Kiislamu kwa kuwapa Waislamu usaidizi dhidi ya Wakristo. Mhusika Mungu ameingiliana na mandhari dhahania ya mbinguni ambako anaishi.

#### 4.2.1.4 Malaika Jibrili

Jibrili ni mhusika asiyeonekana kwa macho ya wahusika wengine ila Muhammadi tu. Ni mhusika msaidizi ambaye ni mjumbe na mshirika wa karibu wa Mwenyezi Mungu. Mungu anamtumia Malaika Jibrili kila mara kuwasiliana na Mtume Muhammadi na kumpa mawaidha na mwelekeo wa kuchukua katika vita vya Tambuka.

Malaika Jibrili amechorwa kama mjumbe mwaminifu kwani kila mara anapotumwa na Mungu kwa Mtume Muhammadi, anamfikishia ujumbe huo kwa njia iliyo wazi na haki. Sababu kuwa yeye tu ndiye anatumwa kunaashiria kuwa yuko karibu zaidi na Mungu.

Malaika Jibrili anatoa mchango mkubwa katika vita vya Tambuka kwani anaunganisha Mtume Muhammadi na Mungu na kuhakikisha kuwa wahusika wa Kiislamu hawachelewi kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu kila anapowataka kufanya hivyo.

#### 4.2.1.5 Mughera

Mughera ni mojawapo wa wahusika wa Kiislamu na mwanajeshi. Ni mhusika mjenzi. Tunakutana naye wakati ambapo Mtume Muhammadi anawataka majehi yake kutunda matango kwa ajili ya safari yao. Tunaona kuwa Mughera anatia shaka moyoni mwake na kufanya kosa la kutupa matango hayo na kubakia na matatu tu. Hata hivyo, Mughera anajuta anapogundua kuwa matunda hayo yanatokwa na asali. Htimaye Mughera anatubu na kusamehewa na Mtume Muhammadi.

Majukumu ya Mughera katika *Utenzi wa Tambuka* ni kuwasilisha maudhui ya toba na msamaha. Vilevile, anatumiwa kuonyesha haja ya Waislamu kuwa na imani na kumwamini Mtume Muhammadi kila mara. Pia, Mughera anatumiwa kuonyesha wasifu wa Muhammadi kuwa mwepesi wa kusamehe.

#### 4.2.1.6 Karari

Karari ni mhusika Mwislamu anayeishi katika jangwa la Hijabu. Ni mhusika mjenzi kwa kuwa anatumiwa kujenga maudhui ya ukarimu na imani ya kidini. Tunaona Karari akikubali kuwapa Muhammadi na jeshi lake bila malipo. Karari anafanya hivi kwa kuahidiwa na Mtume Muhammadi maisha mema ya Peponi.

Karari ni kielelezo cha nguzo ya zakat ya dini ya Kiislamu. Kutokana naye, tunapata funzo kuwa kila Mwislamu anafaa kuwa tayari na kujinyima ili kuendeleza dini hiyo.

#### 4.2.1.7 Mkewe Ali

Mkewe Ali ni bintiye Mtume Muhammadi. Mengi hayajaelezwa kumhusu. Amedokezwa tu mwishoni mwa utenzi anapomkaribisha Ali nyumbani kutoka vitani. Ni mnyenyekevu kwani anambusu Ali na kumwangukia nyayoni kisha kumtoa lebasi.

Ni mwanamke anayepigiwa mfano bora wa wanawake wa Kiislamu. Ni mdadisi. Anapomkaribisha mumewe nyumbani na kumpa kiti, anamuuliza maswali mengi kuhusu vita ambayo Ali anamwelezea. Vilevile, mkewe Ali ni mcha Mungu. Anapoelezewa kuhusu ushindi wa vita anamshukuru Mungu kwa yote.

Mkewe Ali ni mhuska mjenzi kwa kuwa anatumiwa tu kujenga maudhui ya nafasi ya mwanamke katika vita vya Tambuka. Pia ni mhusika mjenzi kwa kuwa anajenga sifa za Ali kuwa mwenye mapenzi ya kweli na mwajibikaji kwa familia yake.

#### 4.2.1.8 Wahusika wa kimakundi wa Kiislamu

Hawa ni wahusika waliokusanyika kwenda vitani chini ya viongozi wao. Wahusika hawa ni wahusika wasaidizi, kwani wamesaidia wahusika wakuu katika kuwasilisha dhamira na ujumbe wa utenzi huu. Wao ni pamoja na Omari, Sayid, Mustafa na wengineo. Kunao wahusika wanaosifiwa wanapokuwa wakiingia Madina kwa matayarisho ya vita. Mtunzi amewataja baadhi yao tu bila kuwajenga. Kwa mfano, Bilali.

Wahusika hawa wa kimakundi wamechorwa kuwa mashujaa. Wanapigana katika vita vya Tambuka kwa ujasiri bila kugopa. Hatimaye, wanaweza kutwaa ushindi kwa usaidizi wa Ali.

Pia, wahusika wa kimakundi wa Kiislamu niwenye imani na wacha Mungu. Tunaona kuwa wanaamini maneno ya Muhammadi kuwa wataenda kuingia Paradiso siku ya Kiyama. Imani yao inaonyesha maudhui ya dini na usufii. Wahusika hawa wameingiliana vyema na mandhari ya jangwani kwani wanaonyesha sifa za uvumilivu wa hali ya juu.

#### 4.2.2.0 Wahusika wa Kikristo

Wahusika wa Kikristo ni wakazi wa Tambuka ambao pia ni wafuasi wa mfalme Herekali. Wahusika wa Kikristo tunaowazingatia katika uhakiki huu ni mfalme Herekali, Askofu Waziri na wahusika wa kimakundi.

#### 4.2.2.1 Mfalme Herekali

Herekali ni mfalme wa Rumu na kiongozi wa Wakristo. Ni mwingi wa ghadhabu. Anapopokea barua kutoka kwa Mtume Muhammadi, papo kwa hapo anamwamuru Asikofu kuandaa jeshi liende vitani. Anaandika barua akimweleza Mtume Muhammadi kuwa yeye yuko tayari kwa vita.

Herekali pia ni mwenye jitihada. Mbali na kuwa jeshi lake linazidiwa vitani, hafi moyo kwa haraka. Anajikakamua na kuendelea kutoa majeshi zaidi kushiriki katika vita dhidi ya Waislamu.

Herekali ni mwenye majivuno. Anapopata barua ya vita anampa Patrikios kisha anaanza kujivuna kuhusu ukuu wake. Anaamuru kasisi kuandaa jeshi kwa vita dhidi ya Muhammadi. Haya yanaonekana katika ubeti wa 133.

Herekali pia amechorwa kama kiongozi shujaa. Tunaona akipambana na Waislamu katika vita vya Tambuka bila kukata tama. Anapigana hadi mwisho. Pia anakubali kuuawa na sio kusilimu.

Herekali anawasilisha maudhui ya ukatili, ukafiri na ushujaa. Pia anasaidia kuendeleza msuko kinzani na hivyo kusaidia kuonyesha sifa za Mtume Muhammadi.

#### 4.2.2.2 Askofu Waziri

Askofu Waziri ni mhusika msaidizi wa Mfalme Herekali. Anasaidia Herekali katika uongozi wa Wakristo. Pia anampa ushauri katika vita vya Tambuka.

Askofu Waziri anaonyesha ustadi katika ushauri wake kwa Herekali kwani anaweza kuendeleza vita vya kishujaa hadi mwisho. Askofu Waziri ni mwaminifu na mzalendo. Tunaona akiwa mwaminifu kwa Herekali na Ukristo hadi mwisho. Hata anakubali kuuawa kuliko kusilimu na kuisaliti dini yake.

Askofu ametumiwa kuwasilisha maudhui ya ushujaa, ukafiri, uaminifu na ukatili. Pia metumiwa kuendeleza msuko kinzani.

#### 4.2.2.3 Wahusika wa kimakundi wa Kikristo

Wahusika Wakristo wa kimakundi ni wanajeshi ambao wanapigana dhidi ya Waislamu katika *Utenzi wa Tambuka*. Ni wahusika wasaidizi kwani wanasaidia Mfalme Herekali kuendeleza upinzani wake vitani. Wahusika hawa ni wengi. Wamechorwa kuwa mashujaa kwani wanapigana kishujaa. Wanaweza kuwashinda Waislamu katika mapigano ya mwanzoni. Wengi wao wanauawa vitani. Kufikia mwishoni mwa vita, wengine wanalazimishwa kusilimu. Wengine wanakataa na wanauawa.

Wahusika hawa pia wamechorwa kuwa makafiri. Tunaona kuwa hawamwamini Mungu. Wanabeba sanamu ambazo ndizo wanazoabudu.

Wahusika wa kimakundi wamewasilisha maudhui ya ukafiri, ushujaa na kifo. Pia wametumiwa kujenga msuko kinzani.

**4.2.3.0 Wahusika wanaobadilika**

Wahusika wanaobadilika ni wale ambao mwanzoni wanapatikana upande mmoja lakini baadaye wanajiunga na upande pinzani.

**4.2.3.1 Jasusi**

Jasusi ni mhusika Mkristo kuanzia mwanzoni mwa utenzi. Jasusi anatumwa na Mfalme Herekali kupeleleza idadi kamili ya majeshi ya Waislamu. Anapofika kwa Muhammadi, Jasusi anakosa kuwasalimu walinzi wa Mtume Muhammadi, jambo ambalo si tabia ya Waislamu kama anavyoeleza mtunzi. Pia Jasusi anagunduliwa kuwa ananuka pombe. Tabia hii inawafanya waamini kuwa Jasusi ni mkristo.

Wakati Waislamu wanapotaka kumwua Jasusi, Mtume Muhammadi anawakanya. Jasusi anasamehewa na kuruhusiwa kurudi kwa Herekali. Anapofika huko, anamweleza Herekali kuhusu uzuri na urembo wa Muhammadi. Herekali anaposikia hivyo, anaamuru Jasusi kuuawa. Kabla ya kufa, Jasusi anakiri kuwa Uislamu ndiyo dini ya kweli na kuwa Mtume Muhammadi ndiye mtume wa Mungu.

Jasusi anatumiwa kama mhusika mjenzi. Anajenga maudhui ya dini. Pia anajenga sifa ya usamehevu na uzuri wa Mtume Muhammadi. Herekali pia anajenga sifa ya ukatili na ukafiri wa mfalme Herekali.

## 4.3 HITIMISHO.

Tumeona kuwa mandhari yanayojitokeza ni ya kijiografia, kidhahania, kimiujiza, kinyumbani, kivita na hata ya mjini. Pia tumeona kuwa wahusika wanaweza kugawanywa katika makundi mawili makuu: kundi la Waislamu na kundi la Wakristo. Kundi la Waislamu linaongozwa na Mtume Muhammadi. Kundi la Wakristo linaongozwa na Mfalme Herekali. Pia kunao wahusika wakuu, wajenzi na wasaidizi.

Pia tumeona kuwa uumbaji wa wahusika umeingiliana na uumbaji wa mandhari na msuko. Wahusika hawa na matendo yao katika mandhari hayo yanasaidia kuwasilisha maudhui na kuendeleza msuko.

**anambialo** badala ya 'aniambialo' (ubeti wa 11), **jamaaze** badala ya 'jamaa zake' (ubeti wa 14), **nduguye** badala ya 'ndugu yake' (ubeti wa 15), **kwambami** badala ya 'kwamba mimi' (ubeti wa 69), **zo** badala ya 'hizo' (ubeti wa 129), **dahabuze** badala ya 'dhahabu zake' (ubeti wa 114), **barakaze** badala ya 'baraka zake' (ubeti wa 1142), **io** badala ya 'hiyo' (ubeti wa 486), **manenoye** badala ya 'maneno yake' (ubeti wa 182).

### 5.1.1.2 Mazida

Mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* ameonyesha umahiri wake katika kuutumia uhuru wa kishairi kurefusha maneno kadha. Hali hii inanuiwa kusawazisha mizani na vina katika shairi. Miongoni mwa maneno yaliyorefushwa ni:

**Sabia** badala ya 'saba' (ubeti wa 15), **Muungu** badala ya 'Mungu' (ubeti wa 24), **Alii** badala ya 'Ali' (ubeti wa 40), **sabuini** badala ya 'sabini' (ubeti wa 257), **Nabiyaka** badala ya 'Nabii' (ubeti wa 219), **alifu** badala ya 'elfu' (ubeti wa 226), **walitozile** badala ya 'walitoa' (ubeti wa 506), **wakeeo** badala ya 'wakeo' (ubeti wa 545), **kawatoseze** badal ya 'kawatoza' (ubeti wa 559), **haufu** badala ya 'hofu' (ubeti wa 545), **kikatooka** badala ya 'kikatoka' (ubeti wa 1047), **kusuudi**, badala ya 'kusudi' (ubeti wa 1055), **ilinipele** badala ya 'ilinipa' (ubeti wa 1147).

### 5.1.1.3 Tabdila

Tabdila imetumika katika utenzi ili kusawazisha mtiririko wa vina. Mara nyingi mbinu hii hujitokeza mwishoni mwa mishororo. Mifano ifuatayo itathibitisha matumizi ya mbinu hii: **Maongoni** badala 'ya miongoni' (ubeti wa 87), **hoyo** badala ya 'huyo' ubeti

# SURA YA TANO

# MATUMIZI YA LUGHA KATIKA *UTENZI WA TAMBUKA*

## 5.0 UTANGULIZI

Sura hii inashughulikia matumizi ya lugha katika utenzi huu. Tunahakiki kipengele cha matumizi ya lugha katika viwango viwili kama tulivyoeleza katika sura ya pili. Tunaanza na uhuru wa kishairi na kisha tamathali za usemi. Kila mara tutatoa mifano kutoka katika utenzi wenyewe.

## 5.1.0 UHURU WA KISHAIRI

Tulieleza uhuru wa kishairi kuwa aina ya ukiushi katika matumizi lugha ambapo mshairi anakuwa na uhuru wa kukiuka kaida za kisarufi za lugha husika.

### 5.1.1.0 Ukiushi wa kimofolojia

Ukiushi wa kimofolojia katika ushairi ni aina ya uhuru wa kishairi ambapo mshairi anaruhusiwa kuyaendeleza maneno tofauti na jinsi ilivyozoeleka katika lugha sanifu. Mshairi ana uhuru wa kurefusha maneno, kuyafupisha au kupangua hijai yake.

### 5.1.1.1 Inkisari

Inkisari ni uhuru unaohusu ufupishaji wa maneno. Mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* amefupisha maneno mengi sana katika utenzi huu. Lengo ni kupata idadi mwafaka ya mizani katika mishororo. Baadhi ya maneno yaliyofupishwa ni kama vile **zikamaa** badala ya 'zikamalizika' (ubeti wa 4), **kanitami** badala ya 'akaniita mimi' (ubeti wa 8),

wa 52, **fahama** badala ya 'fahamu' (ubeti wa 87), **Wangine** badala ya 'wengine' (ubeti wa 15), **Jahanama** badala ya 'jahanamu' (ubeti wa 1140), **Kusikilia** badala ya 'kusikia' (ubeti wa 1138), **Kumubusi** badala ya 'kumubusu' (ubeti wa 1096), **Ondokani** badala ya 'ondokeni' (ubeti wa 26), **Niyilia** badala ya 'nililia' (ubeti wa 8), **Miomoni** badala ya 'midomoni' (ubeti wa 89), **Ruhu** badala ya 'roho' (ubeti wa 97), **Kisisi** badala ya 'kasisi' (ubeti wa 764), **Mungi** badala ya Mwingi (ubeti wa 779), **Kashahadia** badala ya 'Kashuhudia' (ubeti wa 888).

### 5.1.2.0 Ukiushi wa kimsamiati

Ukiushi wa kimsamiati katika ushairi ni aina ya huru wa kishairi ambao unahusu matumizi ya maneno au misamiati mbalimbali ambayo si kawaida kutumika katika katika lugha sanifu. Ukiushi huu unaweza kutokea katika ukopaji wa msamiati, matumizi ya lugha chakavu na maneno kutoka lahaja nyingine.

### 5.1.2.1 Lahaja ya kingozi

Mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* ametumia baadhi ya msamiati wa lugha ya Kingozi. Tutaorodhesha mifano michache ya msamiati wa Kingozi iliyotumiwa na msanii kama ithibati: **khawambile** - nikwambie (ubeti wa 14), **akapulika** - akasikia (ubeti wa 15), **jitendele** - jitendee (ubeti wa 286), **nikupele** - nilikupa (ubeti wa 446), **wawenepo** - walipowaona (ubeti wa 917), **nikutumile** - nilikutuma (ubeti wa 1007), **zakwe** - zake (ubeti wa 4), **wakwe** - wake (ubeti wa 1095), **mato** – macho (ubeti wa 912), **niumbile** - uliniumba (ubeti wa 1085).

#### 5.1.2.2 Lahaja ya Kiamu

Matumizi ya msamiati wa Kiamu kama vile alivyotumia mtunzi yanajitokeza katika mifano ifuatayo:

**Mbwene** (nimeona) ubeti wa 7 , **ndia**(njia) ubeti wa 25 , **pamoya** (pamoja) ubeti wa 25 **mumoya** (mmoja) ubeti wa 822, **undetee** (uniletee) ubeti wa139 **iti** (nchi) ubeti wa 1078 **mbee** (mbele) ubeti wa 1082, **wothe** (wote) ubeti wa 167 , **ndiani** (njiani) ubeti wa166 **yuani** (juani) **ndiaye** (njia yake)ubeti wa 141 **zambi** (dhambi) ubeti wa 80 , **muyini** (mjini) ubeti wa 50

#### 5.1.2.3 Msamiati wa Kiarabu

Katika utunzi wa *Utenzi wa Tambuka*, matumizi ya msamiati wa kiarabu yanajitokeza katika mifano ifuatayo: **kuffari** - kafiri (ubeti wa 439), **kukutubu** – kuandika (ubeti wa 749), **jifiri** -jeshi (ubeti wa 832), **arobata** – arobaini (ubeti wa 832), **ghubari** - vumbi (ubeti wa 82), **nari** - moto (ubeti wa 391), **thalatha mia** - mia tatu (ubeti wa 835), **kidhabu** – mwongo (ubeti wa 109), **Fadhiya / fadia** - fadhili (ubeti wa 285), **sukunu** - hapa (ubeti wa 285), **habibu** – nzuri (ubeti wa 115), **sahaba** - rafiki (ubeti wa 186), **kilabu** - mbwa (ubeti wa 487).

Katika *Utenzi wa Tambuka*, tunaona kuwa misamiati ya Kiarabu imetumiwa na kurudiwa katika beti zifuatazo: ubeti wa 1148, 1149 na 1150. Tutathibitisha katika ubeti ufuatao:

**La ilaha ili' Allaha**

**La ilaha ili' Allaha**

**La ilaha ili' Allaha**

**La ilaha ili' Allah**

Maneno haya yanamaanisha kuwa, hakuna Mungu mwingine ila Allah. Mtunzi ameyatumia maneno haya jinsi yalivyo ili kuhifadhi maana iliyokusudiwa.Yakitafsiriwa maana haitajitokeza jinsi anavyotaka. Huenda pia mtunzi alilenga wafuasi wa Kiislamu, ambao wanaelewa Kiarabu. Kuna nukuu za Kiarabu vilevile kama vile katika ubeti wa 636 kama ifuatavyo:

**Halidi katanabbahi**

**Akamba inna lillahi**

**Maa inna ilaihi**

**rajiuna akikoa.**

Maneno haya husemwa wakati ambapo muumini wa dini ya Kiislamu ameaga dunia. Inadhihirika wazi kwamba katika vita hivi, baadhi ya wanaokufa ni Waislamu. Inabidi wapewe heshima yao kama ilivyo desturi katika dini hii.

### 5.1.3.0 Ukiushi wa kisintaksia

Ukiushi wa kisintaksia unajitokeza katika *Utenzi wa Tambuka*. Maneno yanayostahili kuja mwanzoni mwa sentensi yanakuja mwisho. Tutathibitisha hayo kwa mifano ifuatayo:

**Madina wakawasili** badala ya 'wakawasili Madina' (ubeti 205)

**Wothe wakenda zitani** badala ya 'wakaenda wote vitani' (ubeti wa 332

**Kaka mufahamu** badala ya 'mufahamu kaka' (ubeti wa 856).

**Mwoyowe kuhikimu** badala ya 'kuhikumu mwoyowe' (ubeti wa 774.

**Ndiye muyuzi fahamu** badala ya 'fahamu ndiye mjuzi' (ubeti wa 774

**Ali Madina kilele** badala ya alikuwa 'Madina akilala' (ubeti wa 14).

**Mambo yangu washikapo** badala ya 'washikapo mambo yangu' (ubeti wa 36).

**Kesho wenda kungia** badala ya 'utaenda kuingia kesho' (ubeti wa 221).

**Mafumoni wakatia** badala ya 'wakatia mafumoni' (ubeti wa 658).

**Tumwa ukinitetea** badala ya 'ukimtetea Mtume' (ubeti wa).

**Dini yako tutangia** badala ya 'tutaingia dini yako' (ubeti wa 1109).

**Akamubusi Fatima** badala ya 'Fatuma akambusu' (ubeti wa 1095).

## 5.2.0 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi ni aina ya ukiushi katika matumizi lugha ambapo mtunzi hukiuka maana ya kimsingi ya maneno. Tamathali za usemi ni ukiushi wa kisematiki.

### 5.2.1 Tashbihi / tashbiha

Mbinu hii ya mfanano imetumiwa sana na mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka*. Lengo kuu la kutumia mbinu hii ni kujenga taswira akilini mwa msomaji ili kurahisisha uelewa. Hata hivyo, tutaorodhesha mifano michache kuthibitisha matumizi yake katika utenzi huu. Katika ubeti wa 361, Kikosi cha Banu Hilali kinalinganishwa na nyati mkali aliye tayari kushambulia. Sababu ya kuwalinganisha wahusika hawa na nyati mukali ni kuashiria ushujaa wao.

Katika ubeti wa 497, mbinu ya mfanano imetumika kulinganisha fumo ambalo Omar alitikizatikiza na kulifananisha na ndimi za nyoka. Sababu ya ulinganishi huu ni kuonyesha kuwa wahusika hawa wana vifaa vikali sana vya kivita na hivyo wanaweza kuwashinda Wakristo.

Vilevile, mbio wanazotimua majeshi wa Kikristo vitani katika vita zinalinganishwa na mbio za mbuzi asiye na mchungaji. Tashibihi hii inawachora majeshi hawa wa Kikristo kama waoga na wasio na nguvu. Kutokana na hayo, Wakristo wanashushwa hadhi yao.

Katika ubeti wa 569 kuondoka kwa Asikofu kuelekea Tambuka kunafananishwa na moto uwakao na usioweza kuzimwa. Moto unajulikana kuwa hatari na unaoweza kuharibu mali kwa haraka sana. Kuwafananisha Waislamu na moto ni kuonyesha kuwa wao ni hatari sana na hivyo wao ni mashujaa.

Katika ubeti wa 600, kule kutapakaa kwa jeshi la Warumu baada ya kushindwa na Waislamu vitani kunamithilishwa na kumbikumbi wakichurunia mvua. Ulinganishi huu unanuiwa kuonyesha namna wahusika hawa ni wengi na wana haraka ya kushambulia.

Katika ubeti wa 1003, machozi anayolia Muhammadi yanafananishwa na mvua. Tashibiha hii inaonyesha wingi wa machozi ambayo Muhammadi analia. Tashibiha hii inaonyesha kuwa Muhammadi ana uchungu mwingi sana na hivyo anahuzunikia watu wake ambao wanauawa.

Katika ubeti wa 1070, mbinu ya tashibihi pia imetumika katika kuonyesha jinsi Warumu wanavyoangamizwa na Waarabu mithili ya payayo na nari (nyasi iliyokauka na moto). Tashibiha hii inaonyesha kuwa Waislamu ni hatari sana wakilinganishwa na Wakristo.

Mifano mingine ya tashibiha inapatikana katika beti zifuatazo: 870, 872, 923, 915, 919, 971, 968 na nyingine nyingi.

### 5.2.2 Sitiari

Mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* ametumia mbinu ya sitiari kwa kiwango fulani. Mbinu hii imetumika ili msomaji aweze kufikiria na kufumbua maana iliyokusudiwa na mshairi. Matumizi ya sitiari yanadhihirika katika mifano ifuatayo:

Ubeti wa 773;

Naye **Siraji** Muniri

Ndiye Thumwa munawiri

Kipendi yakwe **Jabbari**

Katika ubeti huu, Mtume Muhammadi anasawiriwa kama taa iangazayo na mwamba imara. Sitiari hii inatumiwa ili kuonyesha kuwa Mtume Muhammadi ni shujaa na vilevile tumaini la Waislamu. Yeye ndiye ajuaye yaliyo mema kwa Waislamu.

Katika ubeti wa 1015, Ali pia anasawiriwa kama simba.

> Ewe **simba** ya Mwelethu
>
> niakwita niyilia

Maneno katika mishororo ya ubeti huu yanatumiwa na Muhammadi akimwita Ali aje kusaidia katika vita. Jina 'simba' linaonyesha ushujaa alionao Ali katika vita. Pia Ali anaitwa **Haidari** kama inavyodhihirika katika ubeti wa 1036.

Katika ubeti wa 539, majeshi ya Kikristo yamerejelewa kama **kilabu**. Yaani, mbwa.

> Wakamwandama **kilabu**
>
> Kama ya thui na paa

Kumrejelea Herekali na majeshi yake kama mbwa kunaonyesha madharau waliyonayo Waislamu kwa Wakristo. Pia inaonyesha hisia za mtunzi kuwahusu.

Mifano zaidi ya sitiari inapatikana katika beti za 1083, 1095, 503, 350 na 220.

### 5.2.3 Tashihisi / uhuishi

Mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* ametumia tamathali hii ya usemi katika utenzi kwa kiasi kidogo. Mbinu hii imetumika ili kumfanya msomaji apate hisia fulani katika kazi anayoisoma. Baadhi ya mifano zilizotumika ni:

Phanga zikitenda kazi, (panga zilitumika kukatakata watu) katika ubeti wa 826.

Nyumba za kiza na nari zikenda kutinikia (Nyumba za kiza na nari zilisababisha mashaka na mateso kwa wale waabuduo sanamu.) katika ubeti wa 835.

Wadhu alifu idadi phepo ikawamukua (watu elfu moja waliaga dunia) katika ubeti wa 833.

Bahari ikaratili na miti ikaomboa (bahari ikaongea na miti nayo ikatabiri) katika ubeti 463

Mifano zaidi zapatikana katika beti za 870 na 470.

### 5.2.4 Maswali ya Balagha

Katika kazi ya kifasihi maswali ya balagha hutumiwa kwa lengo maalum. Msanii ametumia maswali ya balagha kwa kiasi kidogo katika utenzi huu. Nia yake ni kumtaka msomaji aweze kutafakari zaidi juu ya wazo fulani, kusisitiza ujumbe wake na vilevile kuwatia wahusika moyo. Mifano ya kuthibitisha semi hii ni kama ifuatayo:

Katika ubeti wa 54, Mtume Muhammadi anawauliza Wakristo kuwa wanaposoma vitabu vyao vitakatifu hawaoni kuwa yeye ndiye Mtume wa mwisho. Swali hili linalenga kuonyesha kuwa Muhammadi ndiye Mtume wa pekee wa Mungu na hilo linajulikana na kila mtu.

### 5.2.5 Methali

Msanii hajaonyesha umahiri wake katika matumizi ya methali katika utenzi huu. Hii ni kwa sababu inabainika wazi kuwa methali imetumika mara moja tu katika utenzi mzima. Mfano wa mashiko ni katika ubeti wa 373. Methali yenyewe ni:

**Yapisiliyo ya nyuma**

**tumazie yasukuma**

(Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo)

Methali hii imetumika kwa nia ya kuwahimiza wapiganao. Hawastahili kufa moyo hata wanapoonekana kushindwa kwani wakijikaza ushindi ni wao.

### 5.2.6 Nidaa

Mtunzi ametumia nidaa kwa uchache sana kwa nia ya kuwahimiza na pia kuonyesha hisia mbalimbali za wahusika wake. Mifano katika utenzi huu inapatikana katika ubeti wa 133:

**Mulio koko toshani!**

**Sihitajimu kungia.**

Tunaona kuwa Herekali anaambia Askofu kuwa wao wanatosha na wana uwezo wa kupigana dhidi ya jeshi la Muhammadi na washinde. Anawahimiza kwa kumaka kuwa wanatosha na hivyo yeye hastahili kujiunga nao.

Mfano mwingine unapatikana katika ubeti wa 795:

**Jamaa za Herekali**

**Wakawajibu kauli**

**Haya! Hatutayakubali**

**hatu wenye kutikia .**

Katika ubeti huu nidaa imetumika kuonyesha msimamo wa majeshi ya Waislamu na kusisitiza kuhusu jambo fulani.

### 5.2.7 Takriri

Mbinu ya takriri inajitokeza katika viwango mbalimbali. Kuna takriri za neno vilevile za sauti fulani. Mtunzi ametumia takriri katika kazi hii kwa sababu anataka kusistiza ujumbe fulani kwa msomaji. Baadhi ya takriri zilizotumika ni kama ifuatavyo:

**Han**a muke **hana** mwana ubeti wa 68. Usemi huu unatumiwa kumrejelea Mungu ambaye msimulizi anasisitiza kuwa Mungu hana mfano wake kama wanavyoelezea Wakristo.

Katika ubeti wa 82, tunaelezwa kuwa "Hattari akaradidi**.** Pia katika ubeti wa 98, tunapata takriri **u** radi nami **u** radi, Hatari akakariri ubeti wa 169, Kaokota **ganda ganda** (ubeti wa 301), **Pap**ale uk**ipepe**a (ubeti wa 375), utakataka (ubeti wa 376/377), Sawasawa (ubeti wa 502), undetee himahima (ubeti wa 1390, hapa na hapa (ubeti wa 600), Fumole kisukasuka (ubeti wa 497), Asikafu kakariri (ubeti wa 110), Kitakoni

sawasawa (ubeti wa 47), muthu **mumoya mumoya** (ubeti wa 911), **Labbaika labbaika** (ubeti wa 1021).

Beti za 1148, 1149, 1150 zinafanana, sehemu hii imerudiwarudiwa.

**La ilaha ili Allaha**

**La ilaha ili Allaha**

**La ilaha ili Allaha**

Tunaona kuwa katika baadhi ya beti takriri za irabu zimejitokeza. Tutaonyesha katika mifano ifuatayo:

Ubeti 7.

Mbwene fumo kuitak**a**

Haidioi ya Nabiyak**a**

Aiwenepo Tambuk**a**

Muno ikamujibi**a**

Ubeti wa 701

Herekali kipulik**a**

Kwamba thumwa u Tambuk**a**

Alimazie kuulik**a**

Haima kuikali**a**

Ubeti 1142

Wenye kunipa maan**a**

ya utendi kulingana

wapeekwe fi li janna

kwa barakaze Rasua.

Mifano zaidi inapatikana katika beti hizi: 432, 433, 11, 23, 49, 68, 86, 88, 90, 92, 98, 99, 121, 151, 152,140

### 5.2.8 Chuku (Udamisi)

Mbinu hii imetumika na mtunzi katika utenzi wote kuhusu vita kati ya Waarabu na Wakristo. Wasanii hutumia chuku kutilia mkazo wazo fulani au hata kuchekesha. Mtunzi ametumia chuku ili kusisitiza ujumbe alio nao na pia kumtia msomaji shauku ya kuendelea kuisoma kazi ya kifasihi. Kwa mfano, mtunzi anapotuambia kuwa Muhammadi aliita makabila yote ya nchi ya Uarabu na zikaitikia mwito. Hali hii si kawaida maanake si kila mtu anaweza kuitikia mwito wowote ule. Hata katika sherehe za harusi watu hualikwa lakini wanakosa kufika. Katika maisha halisi, lazima kuwepo na upinzani wa hapa na pale. Huenda mtunzi alitumia chuku katika hali hii kuonyesha msomaji umaarufu ambao Mtume Muhammadi yuko nao.

Katika ubeti wa 622, tunaambiwa kuwa watu walipigana vita kwa siku tatu mfululizo mpaka vumbi likajaa na kuunda wingu na mchana ukageuka usiku. Usemi huu ni chuku tu. Haiwezekani kwani binadamu huchoka. Katika hali halisi mtu hawezi kupigana kwa muda huo wote bila kupumzika.

Kisa cha Karari kuwakaribisha wageni sabini na saba elfu ni udamisi. Katika uhalisia wa maisha, kukaribisha wageni kama hao au pengine wachache mtu huanza kujiandaa mapema. Makaribisho ya Karari ni ya ghafla. Vilevile, Karari anawezaje kuwakimu watu hao kwa malazi?

Vilevile, ni chuku kwa mtu kuishi pekee katika mji. Mtunzi ametuelezea kuwa pale Wangwa wa Hijabu paliishi mtu mmoja peke yake. Mtu huyo ni Karari. Haya yanaelezwa katika ubeti wa 400-422.

Tukirejelea kitendo cha mtumwa mmoja katika utenzi huu, kinadhihirisha matumizi ya chuku. Katika maisha halisi watu hutorokea mbali sana mahali penye vita hasa ikiwa silaha kali zinatumika. Ajabu ni kwamba, mtumwa anakwenda katikati ya uwanja wa vita ambapo vita ni vikali sana. Kisa na maana, anataka kuhakikisha kuwa amemuona Ali na hata kumuuliza jina lake. Haya yanasimuliwa katika beti za 1050-1060.

### 5.2.9 Visawe

Mtunzi ametumia visawe vingi katika utenzi huu. Visawe hivi vimetumika kuwarejelea Mungu, Mtume Muhamadi na mfalme Herekali.

Msanii ametumia visawe kwa nia ya kuonyesha ujuzi alio nao katika lugha. Vilevile, anaepuka kuwachosha wasomaji wake kwa kurudiarudia majina yaleyale kwani huchosha akili. Visawe pia ni mbinu ya kujenga sifa za wahusika na kuwasilisha maudhui fulani.

Visawe vilivyotumika katika *Utenzi wa Tambuka* ni kama ifuatavyo:

**Visawe vya Mungu**

Visawe vya Mungu ni vingi na vimetumiwa kwote katika utenzi huu. Visawe vyenyewe ni pamoja na: **Muungamu** - kukiri / kuungama (ubeti wa 20), **Dayyani** (ubeti wa 269), **Mola Latifu** (ubeti wa 4), **Mwenye ezzi** (ubeti wa 23), **Subuhana** (ubeti wa 23), **Bismillahi** (ubeti 44), **Muweza** (ubeti wa 422), **Mannani** – mlipaji (ubeti wa 830), **Wadudi** (ubeti wa 33), **Jalali** (ubeti wa 75), **Karima**, **Mola Jabbari** (Mwamba), **Mola Taa** – aliyetukuzwa (ubeti wa 44), Hallaki – muumba (ubeti wa 46), **Rabbuka** - bwana wako (ubeti wa 421). Visawe vya Mungu ni njia ya msanii ya kutaka kuonyesha sifa ya utukufu wa Mwenyezi Mungu. Hakuna mwingine aliye na majina ya sifa kuu kama alivyo Mungu.

**Visawe vya Mtume Muhammadi**

Visawe vya Muhammadi pia ni vingi mno. Visawe vyenyewe ni pamoja na: **Habibu** – mpendwa (ubetu wa 25), **Nabii** - Mtume (ubeti wa 40), **Thumwa** – mtume (ubeti wa 38), **Ndombezi** – muombezi (ubeti wa 57), **Rasuli** - Mtume (ubeti wa 204), **Siraji Muniri** –mwangaza (ubeti wa 773), **Amini** - aliyeaminiwa (ubeti wa 685). Majina haya ya Muhammadi yanatumiwa kumpa sifa na kujenga maudhui yanayohusiana na sifa zenyewe.

**Visawe vya Mfalme Herekali**

Mfalme Herekali amerejelewa kwa visawe vichache. Visawe vyenyewe si vilivyozoeleka na hivyo vinaonekana kuwa lakabu. Visawe vya Herekali ni pamoja na: **Kilabu** - mbwa (ubeti wa 487), **Juhhali** – mjinga (ubeti wa 834), **Mbugudhu Jalali** – msumbufu / anayeudhi (ubeti wa 51), **Musirika** - asadikiye miungu (ubeti wa 49). Visawe vya Herekali vinaonyesha mtazamo hasi wa msimulizi na vilevile wahusika wa Kiislamu kuwahusu wahusika wa Kikristo.

### 5.2.10 Misemo

Katika utenzi huu, mtunzi hajatumia misemo kwa wingi. Hata hivyo, tutaorodhesha misemo michache iliyotumiwa kama ithibati.

**Kashika ndia** - kuanza safari (ubeti wa 457).

Na **ndaa ikamupata**, alina khiu kuteta (ubeti wa 448). Hii inamaanisha kuwa alikuwa na hamu ya kupigana.

**Osha moyo taghayuri** - kuondoa huzuni moyoni (ubeti wa 1006).

### 5.2.11 Ukinzani / usambamba

Tunaona kwamba katika utenzi huu, mtunzi ametumia mbinu ya ukinzani kwa nia ya kusisitiza jambo. Kwa mfano:

Katika ubeti wa 68, msimulizi anasema '**Hana muke hana mwana**'. Maneno haya yanatumiwa kusisitiza kuwa Mungu si mfano wa binadamu kama wanavyodai Wakristo.

Ukinzani huu unawasilisha maudhui ya imani ya kidini. Mbinu nyinginezo za ukinzani zinazotokea katika utenzi huu ni kama zifuatazo:

Kwa mafumbo kwimiana, **wazee kwa wavulana** (ubeti wa 33).

Yaso **baridi na harri** (ubeti wa 465).

Kupijana kwa **matana kuwa siku na matana** (ubeti wa 603).

**Kungumi-ngumi na kiza** pasikuwa na **mwangaza** (ubeti wa 62)

Tana za **mbele na nyuma** (ubeti wa 825).

**Waumini na Warumu** (ubeti wa 831).

Wakiwana kwa shauku kwa **mutana na usiku** (ubeti wa 967).

Pasi kuwa na mangine illa **kufa na kukia** - pasipo kuwa na mengine ila kufa na kuishi (ubeti wa 868).

### 5.2.12 Tanakali za sauti

Baadhi ya tanakali za sauti zilizotumiwa katika *Utenzi wa Tambuka* ni: yali mwimo na **matozi mitilizi mitilizi** (ubeti wa 18).

kulla muthu kangoroma ( ubeti wa181).

Sayari akatetema ( ubeti wa 496).

Farasi ili kupita, zisizo wathu zikemeta ( ubeti wa 470)

Mtunzi ametumia tanakali kwa nia ya kusisitiza.

### 5.2.12 Taashira

Mtunzi ametumia mbinu ya taashira kwa uchache sana. Nia yake kuu ni kuficha maana na hisia mahsusi katika kazi za utenzi huu. Ishara zinazojitokeza wazi katika *Utenzi wa Tambuka* ni:

**Nyumba za kiza na nari** zinazotajwa katika ubeti wa 835 zinaashiria makaburi. Nyumba za kiza zinarejelea kaburi la Mwaarabu ilhali nyumba za nari zinarejelea kaburi la Mrumu. Pia hali hii inarejelea mpaka ulioko kati ya Warumu na Waarabu. Taashira hii inaonyesha imani ya dini ya Kiislamu katika utenzi huu kuhusu hatima ya Wahusika wa Kiislamu na vilevile Wakristo.

Kuhusu kifo cha Sayari, Msanii anatuelezea katika ubeti wa 504 ya kwamba:

> **Ruhu yakwe maleuni**
> **ikapelekwa motoni**
> **nyumbani tahanani**.

(Roho yake aliyelaaniwa ilipelekwa motoni katika kaburi la majuto au mateso. Maleuni vilevile ni jina linaloashiria Mkristo.) Tunaona kuwa **nyumbani** ni ishara ya kaburi alimozikwa Sayari. Kwa upande mwingine mshairi ametumia **tawi la taka** kama ishara. Tawi la taka lililonyoka kabisa linaashiria kifo cha Sayari. Yaani, mwili wake unalinganishwa na jinsi tawi linavyokauka na kukunjana hata kupoteza rangi yake ya kibichi ndio vivyo hivyo Sayari anavyoyapoteza maisha yake.

Katika ubeti wa 547, **kuanguka nyayoni** pa Waislamu ni ishara iliyotumika na mshairi kuonyesha kusalimu amri kwa Warumu na kukubali kushindwa. Wanaonyesha unyenyekevu wao hata wanakiri imani ya Kiislamu. Kama ilivyo desturi ya Kiislamu, iwapo mtumwa atakiri na kusema shahada basi hatauawa.

Ishara hii ya kuanguka nyayoni pia imetumika na mtunzi kuonyesha unyenyekevu alionao Fatuma kwa mumewe Ali. Anaporudi nyumbani kutoka vitani, Fatuma anamwangukia nyayoni, anambusu na hata kumtoa lebasi. Hatimaye, anataka kujua habari zaidi kuhusu vita. Fatuma anapigiwa mfano wa mwanamke mwema wa Kiislamu anavyotakikana awe mnyenyekevu. Haya yanasimuliwa katika beti za 1094 – 1101.

Katika ubeti wa 1117, kuna matumizi ya taashira ya **kalamu** kama ifuatavyo:

> **Ikawa kwisa kalamu,**
> **ya Rasuli na Warumu,**
> **ipisileo hukumu,**
> **nimalizie kawambia.**

Mtunzi ametumia **kwisa kalamu** kuashiria kule kuhitimisha usimulizi wake wa vita kati ya Warumu na Waarabu.

## 5.3 HITIMISHO.

Sura hii imechunguza matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Tambuka*. Uchunguzi umeonyesha kuwa lugha iliyotumiwa ni ya kishairi. Viwango viwili vya matumizi lugha vinavyotumiwa ni uhuru wa kishairi na tamathali za usemi. Vipengele mbalimbali vya matumizi lugha vimeingiliana na mandhari na muundo wa utenzi huu. Pia vimetumiwa kuwasawiri wahusika na kukuza maudhui.

# SURA YA SITA

# TATHMINI NA MAPENDEKEZO

## 6.0 UTANGULIZI

Katika Sura hii tumejadili kwa ufupi matokeo ya utafiti wetu. Matokeo haya ndiyo yatakayotuwezesha kuzipima nadharia tete tulizotaja mwanzoni pamoja na malengo yetu. Mwishowe tunatoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

## 6.1 MUHTASARI WA UTAFITI

Katika utafiti huu tuliazimia kuangalia jinsi mshairi alivyotumia fani mbalimbali na kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Tumeigawa tasnifu katika sura sita.

Sura ya kwanza ilihusu utangulizi wa utafiti. Katika sehemu hii tulielezea maswala ya utangulizi au ya kimsingi ya utafiti wetu. Maswala hayo ni pamoja na maada ya utafiti, tatizo la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete, malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti.

Katika sura ya pili, tumetaja na kutoa fasili za vipengele mbalimbali vya kifani. Pamoja na hayo, tumetolea mifano ya kijumla ya vipengele vya kifani tulivyotaja.

Katika sura ya tatu, tumehakiki msuko na muundo wa *Utenzi wa Tambuka*. Tumeona kuwa utenzi huu una msuko changamano au wa msago. Pia muundo wake wa nje umefuata kaida za utunzi wa tenzi.

Katika sura ya nne, tumehakiki mandhari na wahusika katika *Utenzi wa Tambuka*. Tumeona kuwa mandhari yake ni mchanganyiko. Kuna mandhari ya uhalisia, ya kijiografia, ya kimiujiza, ya mjini, ya mashambani na ya kidhahania. Wahusika ni wa Kiislamu na wa Kikristo. Pia kuna wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi.

Katika sura ya tano, tumehakiki matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Tambuka*. Vipengele vya matumizi lugha tulivyojadili ni uhuru wa kishairi na tamathali za usemi. Tumeona kuwa mtunzi ametumia uhuru wa kishairi na tamathali za usemi kwa wingi na kwa ufundi. Matumizi ya lugha yamesaidia kukuza maudhui, mandhari na kusawiri wahusika.

Utafiti wetu umetupelekea kutambua kuwa *Utenzi wa Tambuka* umejengeka kwa misingi ya fani. Msanii amefaulu katika matumizi ya fani mbali. Tumethibitisha matumizi ya Kiamu na Kingozi. Kiarabu vilevile kimetumika. Hii ni kwa sababu, utenzi huu unahusu vita kati ya Warumu na Waarabu. Kwa vile Kiarabu ndiyo lugha ya kimsingi ya dini ya Kiislamu, mwandishi hakuwa na budi kuitumia. Kiarabu kimetumiwa katika sehemu chache bila kutafsiriwa. Ilichukuliwa kwamba Mwislamu atafahamu lakini tumegundua kuwa utenzi huu ni wa manufaa kwa msomaji yeyote. Matumizi ya lahaja yamechangia pakubwa sana utajiri wa msamiati katika utenzi huu. Kwa upande wa mbinu za utunzi, mwandishi ameonyesha umahiri wake wa kutumia tamathali kadha za usemi ili kuwasilisha ujumbe. Matumizi haya yamewezesha kazi hii

kuvutia sana msomaji. Isitoshe, kazi hii inachangia pakubwa katika tawi la fasihi kwa jumla.

Kwa kuchunguza wakati ambapo utenzi huu ulitungwa, tumegundua ya kwamba mtunzi alikuwa na umahiri mkubwa sana katika matumizi ya lugha. Kupitia kwa kipengele hiki tunaona ya kwamba mtunzi ameonyesha ustadi wake wa kujenga fani katika utenzi huu. Fani iliyojengwa ina uamilifu wake katika matumizi ya lugha ya kisasa kwani haijapitwa na wakati.

## 6.2 KUHUSU MALENGO YA UTAFITI

Kwa upande wa malengo yetu tumebainisha yafuatayo:

Mtunzi Bwana Mwengo bin Athumani, ameonyesha umahiri wake katika matumizi ya lugha. Mbali na uhuru wa kishairi, ametumia aina mbalimbali za tamathali za usemi.Vilevile ametumia mpinduo sarufi kuleta tofauti katika matumizi ya lugha ilivyozoeleka. Hali hii itachangia pakubwa sana matumizi ya lugha katika mtalaa wa fasihi. Matumizi ya lahaja za pwani pamoja na Kiarabu inadhihirika. Matumizi haya yana manufaa zaidi katika ukuzaji wa msamiati katika lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Kuhusu mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya kifani,tumegundua ya kwamba vipengele hivi vinaingiliana na kukamilishana.Tumejadili jinsi ambavyo mandhari yanavyoingiliana na usawiri wa wahusika ili kuwasilisha ujumbe wake mtunzi kwa hadhira.Vilevile tumejadili jinsi msuko na muundo kama vipengele vya kifani vinavyohusiana na kukamilishana ili kuunda kazi nzima ya kifasihi.

Tumegundua ya kwamba msuko katika utenzi huu ni changamano. Hivi ni kumaanisha ya kwamba matukio hayatiririki kwa njia ya moja kwa moja. Kuna misuko mingine ambayo msanii anatumia na inaathiri mfululizo wa msuko mkuu. Hata hivyo, tumetambua ya kwamba misuko hiyo pia ina mchango mkubwa kwenye msuko mkuu.

## 6.3 KUHUSU NADHARIA TETE

Haipothesia zetu zilikuwa mbili:

Kwanza, tulichukulia kwamba mtunzi wa *Utenzi wa Tambuka* ana ukwasi wa mbinu za kifani na kwamba unadhihirisha umbuji wa hali ya juu. Tumethibitisha nadharia tete hii kuwa na mashiko. Tumeona kuwa mtunzi wa utenzi huu ametumia fani kwa ufundi sana.

Pili, tulichukulia ya kwamba vipengele mbalimbali vya kisanaa vinavyotumika katika *Utenzi wa Tambuka* vimechangia pakubwa katika muundo wa umbo la utenzi wenyewe. Tuliweza kuona kuwa nadharia tete hii ni ya kweli. Vipengele vya kifani vilivyotumika vimeingiliana na kukamilishana na kuunda utenzi mmoja wenye mshikamano.

## 6.4 MAPENDEKEZO YA UTAFITI ZAIDI

Utafiti wetu umejikita katika uhakiki wa kifani katika *Utenzi wa Tambuka*. Kuna haja ya kufanyia utenzi huu uhakiki wa kimaudhui. Kwa kuangazia maudhui tutakuwa tumevuka upeo wetu.Vilevile, kipengele kimoja cha fani kinaweza kufanyiwa uhakiki wa kina kwa undani zaidi.

Iwapo utafiti wa baadaye utachunguza maudhui na vipengele vya kifani kwa undani basi wasomi wa siku zijazo watafaidika zaidi. Isitoshe, utafiti wenyewe utauboresha mtalaa wa kifasihi. Hii ni kwa sababu wasomi watakopa baadhi ya msamiati uliotumiwa katika utenzi.

*Utenzi wa Tambuka* ulitungwa enzi za zamani sana. Uhakiki wa siku zijazo unapaswa kulinganisha fani katika utenzi huu na tenzi za sasa. Hali hii itawezesha wasomi kutambua hatua ambazo Kiswahili kimechukua kufikia wakati huu.

Katika uhakiki wetu tumetumia nadharia ya Umuundo. Katika kuchunguza kipengele cha usimulizi peke yake, nadharia ya Naratolojia inaweza kutumiwa vilevile. Nadharia hii itafaa sana kwa sababu utenzi huu ni usimulizi wa matukio ya kihistoria.

# MAREJELEO


Abedi, K. A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: KLB.

Culler, J. A. (1975) *Structuralist Poetics*. London: Routledge & Kegan Paul.

Dorsch T. S. (1965) *Aristotle / Horace / Longinus: Classical Literary Criticism*. Hardsmondsworth.

Earlich, V. (1969) *Russian Formalism*. 3rd Edition. The Hague: Mounton & Co. N. V. Publishers.

Habwe, J. na Karanja, P. (2007) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Knappert, J. (1967) *Traditional Swahili Poetry: An investigation into the concept of East African Islam as Reflected in the Utenzi Literature*. Leiden: E. J. Brill.

__________ (1971) *Swahili Islamic Poetry*. Leiden: E. J. Brill.

__________ (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Darf Publishers.

Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.

Mbatiah, M. (2002) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard Textbooks Group and Publishing.

Mgullu, R. S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Stigand, C. H (1915) *A grammar of Dialectic Changes in the Kiswahili Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

TUKI (1981 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford.

Wafula na Njogu, K. (2007) *Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

_____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

_____________ (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers Ltd.

wa Mutiso, K. (mhariri) (2005) *Utenzi wa Hamziyya*. Dar es Salaam: TUKI.

Wesah, E. (2005) "Uhakiki wa Kifani katika *Utenzi wa Mwana Fatuma*". Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Nairobi.